**Jumamosi Februari 29, 2020** Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580167

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



## Mbunge ahoji kuyeyuka kwa mil. 800/- kodi wawekezaji

UKURASA 3




UKURASA 13

# YAMETIMIA

• **Membe** afukuzwa uanachama CCM, mwenyewe anena... Kinana aonywa, Makamba mambo shwari...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**HAKIMU AKWAMISHA KESI VIGOGO ACACIA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imepiga kalenda...

UKURASA WA 4

**DPP AAGIZA MAHABUSI 85 WAACHIWE HURU**

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, ameagiza mahabusi...

## Waziri apiga 'stop' polisi kukamata bodaboda

UKURASA 3



## BoT yazibana benki riba kandamizi za mikopo

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

MICHEZO YANGA, ALLIANCE HAPATOSHI BARA UK.32 MAONI, KATUNI UK.6

# BoT yabana benki kwa riba kandamizi mikopo

**Na Enock Charles**

BENKI Kuu (BoT) imeanzisha Kanuni za Ulinzi wa Mlaji wa Huduma za Kifedha ili kuwalinda wateja dhidi ya riba kubwa katika mikopo inayotolewa na benki nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Gavana wa BoT, Profesa Florens Luoga, alisema wameanzisha kanuni hizo ili kuwe na ushindani katika benki na kuzuia taasisi hizo kukubaliana kuanzisha au kutoa huduma za kumuumiza mlaji wa huduma zao.

"Sisi tunawawekea sasa kanuni, tunataka wewe unapoendesha huduma, usibague, usiwe na 'practices' (matendo) zisizotenda haki kwa wateja wako. Uwe na huduma ambazo zinamsaidia mlaji.

"Benki zinaweza kukaa pamoja na kukubaliana 'hawa wateja wetu, hawa wafungwa wetu, tuwe na riba ya kiwango fulani'.

Gharama za utawala zinatengenezewa kitu ambacho ni maumivu sana kwa mlaji.

"Hata mikataba ya mikopo inapoandaliwa, kunakuwa na maandishi madogo na lugha inayochanganya kiasi kwamba ukija kusoma unakuwa umechoka, unaamua 'ili nisikose mkopo, bora nisaini," alisema.

Alisema kwa sasa benki zote nchini zitalazimika kutia saini kanuni hizo zinazolenga kumsaidia mwananchi pale anapochukua fedha benki kwa ajili ya matumizi au mkopo kuhakikisha hapatakuwa na tozo na riba kubwa kupita kiasi.

Profesa Luoga pia aliwataka wananchi kutunza fedha ili kuiepushia serikali gharama ya kutoa fedha mpya mara kwa mara kutokana na zilizoko katika mzunguko kuchafuka na kuchakaa.

Alisema fedha zinachakaa haraka kutokana utunzaji usiofaa wa fedha au kuharibiwa kwa makusudi.

Profesa Luoga alisema kupitia sera ya sarafu safi ya BoT ni wajibu wa kila mwananchi kutunza fedha ili itumike kwa muda mrefu bila kuharibika na ni kosa kisheria kuharibu kwa makusudi fedha kwa kuwa inatumiwa na watu wote.

"Matumizi ya pesa yanahitaji uangalifu mkubwa sana na ni vizuri nitumie nafasi hii kuwaasa wananchi kuwa utumiaji wa pesa ambao hauendani na matakwa ya kisheria ni kosa la jinai.

"Kwa mfano, kuna watu wanaoandika kwenye pesa au wanaziweka chini kwenye unyevunyevu, ni vizuri wananchi wakaiheshimu noti ya nchi yetu," alisihi.

Alisema pesa ya Tanzania inatengenezwa kwa ubora wa hali ya juu kwa kutumia pamba kwa asilimia 100 kulinganisha na fedha nyingine kama Dola ya Marekani ambayo hutengenezwa kwa pamba asilimia 75.



Rais Dk. John Pombe Magufuli, akiwa na Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir Bin Ali (katikati), na viongozi wengine waandamizi wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), akitembezwa kukagua maendeleo ya Ujenzi wa Msikiti wa Bakwata, unaojengwa kwa ufadhili wa Mfalme Mohamed wa Sita wa Morocco, Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum. **PICHA: IKULU**

# Membe afukuzwa CCM

**Na Romana Mallya**

YAMETIMIA! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya jana aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Benard Membe, kufukuzwa uanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Chama hicho kimeeleza sababu zilizousukuma kuchukua uamuzi huo dhidi ya kada wake huyo aliyetinga tano bora kati ya watia nia 38 wa kuwania nafasi ya urais mwaka 2015, kuwa mienendo yake katika kipindi cha miaka mitano.

Kamati Kuu ya Halmashauri ya Taifa ya CCM iliyoketi jana, iliazimia Membe kufukuzwa uanachama baada ya taarifa ya ndani ya chama hicho kuonyesha mwenendo wake kutoka mwaka 2014 ambapo katika chama amewahi kupata adhabu nyingine ambazo zingemsaidia kujirekebisha lakini imeonekana sivyo.

Akitangaza uamuzi huo jana jijini Dar es Salaam, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, aliwaambia waandishi wa habari kuwa hayo yametokana na maazimio ya kamati baada ya kufuatilia mienendo ya wanachama wake.

"Uamuzi huu umekuja baada ya taarifa za ndani ya chama kuonyesha mwenendo wake kutoka mwaka 2014 ambapo katika chama amewahi kupata adhabu nyingine ambazo zingeweza kumsaidia kujirekebisha, lakini imeonekana sivyo," alisema.

Polepole alisema katika kikao hicho ambacho kilikuwa na ajenga nne, mojawapo ikiwa kupokea taarifa ya Kamati Ndogo ya Udhibiti na Nidhamu iliyomhoji Membe na makatibu wakuu wastaafu, Yusuph Makamba na Abdulrahman Kinana hivi karibuni kuhusiana na tuhuma za utovu wa nidhamu zilizokuwa zinawakabili.

Alisema kamati hiyo ndogo inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Philip Mangula, ilijadiliwa na Kamati ya Usalama na Maadili ya Taifa iliyo chini ya Mwenyekiti, Rais John Magufuli.

"Kamati Kuu katika kikao chake cha leo (jana) imejadili kuhusu wanachama watatu, Kamati Kuu iliwaona wana tuhuma za kukosa maadili kwa mujibu wa Katiba ya CCM, kanuni za uongozi na maadili na desturi za chama tawala," alisema. Polepole alisema Kamati Kuu imeazimia kwa kauli moja kwamba Membe afukuzwe uanachama wa chama hicho.

Alisema adhabu ndani ya CCM zimegawanyika katika makundi mawili ya siri na ya wazi, akifafanua kuwa adhabu ya karipio na ya kufukuzwa husomwa hadharani.

**MEMBE ANENA**

Muda mfupi baada ya kutangazwa kwa adhabu dhidi yake, Membe aliandika katika ukurasa wake wa Twitter akisema: "Watanzania wenzangu, nimepata habari ya kufukuzwa kwangu kutoka kwenye chama changu cha CCM. Simu zinamiminika hadi nashindwa kuzijibu. Tulieni! Nitapata muda wa kuongea na wote muda si mrefu!"

Kuhusu Kinana, Polepole alisema Kamati Kuu imepokea maelezo na kuazimia apewe adhabu ya karipio kwa mujibu wa kanuni za uongozi na maadili toleo la mwaka 2007. "Adhabu na karipio imeainishwa katika kanuni na inasema 'mwanachama anayefanya kosa linalokipaka matope chama na bila kuonyesha nia ya kujirekebisha, basi Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya taifa inaweza kumpa adhabu ya karipio'.

"Mwanachama aliyepewa adhabu ya karipio, atakuwa katika hali ya matazamio kwa muda usiopungua miezi 18 kutoka leo.

"Mwanachama akiwa katika kipindi hicho hatakuwa na haki ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi katika chama, lakini atakuwa na haki ya kupiga kura kuchagua viongozi wake wa chama kama ana dhamana hiyo," alisema.

Kuhusu Mzee Makamba, Polepole alisema Kamati Kuu imeamua kumsamehe makosa yake baada ya kuandika barua ya kuomba msamaha.

"Kamati Kuu ya Halmashauri ya Taifa imeazimia kufuatilia mwenendo wake, imeazimia kwa kauli moja kwamba Mzee Yusuph Makamba amesamehewa.

"Katibu Mkuu ametoa msamaha huu kwa msingi kwamba Mzee Makamba wakati wote tangu aliposomewa mashtaka yake, amekuwa mtu muungwana na kuomba asamehewe makosa yake kwa barua ambazo zimeambatanishwa kwenye maelezo yake," alisema.

Alisisitiza kuwa kujiunga CCM ni mchakato na kujitoa kuna utaratibu sawa na ilivyo katika kufukuzwa uanachama wa chama hicho kilichoanzishwa Februari 5, 1977.


MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki tajwa hapo juu kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili. Minada hii itafanyika kama inavyoonesha hapa chini kwenye jedwali;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | HAPPY JOHN LEOLE (TAWI LA KARIAKOO) | HAPPY JOHN LEOLE | GARI TOYOTA RAVA4 YENYE NAMBA ZA USAJILI T 813 CLJ (KILITIME) – TABATA CHAMA | 16/03/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 002 | WINFRIDA ANDREW TUPA (TAWI LA ILALA) | MR AND MRS ANDREW TUPA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO KIMARA BARUTI – WILAYA YA UBUNGO | 18/03/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 003 | REIFRIDA CHARLES MGUDE (TAWI LA ILALA) | MARY FRANCIS NGUMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA SARANGA KATA YA SARANGA - WILAYA YA UBUNGO | 18/03/2020 SAA 08:00 MCHANA |
| 004 | HUBERT APOLINARY MUSHI (TAWI LA KARIAKOO) | MWANAISHA IBRAHIM HAJI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO ENEO LA CHARAMBE MBAGALA – WILAYA YA TEMEKE | 20/03/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 005 | RAZAK POUL MKANYA (TAWI LA KARIAKOO) | SALUM HAMISI MKUNGU | NYUMBA ISIYOKAMILIKA (SEMIFINISHED HOUSE) YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA KONDOGWA – WILAYA YA TEMEKE | 20/03/2020 SAA 08:00 MCHANA |
| 006 | MAUA RASHIDI DILANGIRE | MAUA RASHIDI DILANGIRE | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA MGEULE – WILAYA YA ILALA | 23/03/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |

**Masharti ya mnada**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo na mahali iliko.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

**KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NA:**

**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, AU Maseto Auctioneer,**
**MKURUGENZI MTENDAJI, MKURUGENZI MTENDAJI,**
**P.O BOX 669, P.O BOX 75087,**
**DAR ES SALAAM DAR ES SALA**
**Tel+255 02221183403 +255 765 999 000 AU +255 787 288 442 AU +255 762 260 787**

## Hakimu akwamisha kesi vigogo Acacia

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imepiga kalenda kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili rais wa zamani wa migodi ya Pangea, North Mara, Exploration na Bulyanhulu, Deogratius Mwanyika, na wenzake mpaka Machi 13, mwaka huu.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi, Vicky Mwaikambo baada ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Godfrey Isaya, kuwa na udhuru.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai mahakamani kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na Hakimu Isaya amepata udhuru, hivyo upande wa utetezi kama una hoja za kuwasilisha, usubiri tarehe nyingine.

Mapema mahakamani hapo, upande wa utetezi ulidai kesi hiyo inahusiana na makubaliano yaliyotiwa saini hivi karibuni kati ya Serikali na Kampuni ya Barrick kuashiria kumalizika kwa mgogoro uliokuwapo awali.

"Mheshimiwa Hakimu, kesi hii ina uhusiano na makubaliano yaliyotiwa saini kati ya Serikali na Kampuni ya Barrick na vyombo vya habari vimeripoti kumalizika kwa mgogoro baina ya pande hizi kwa kuanzishwa Kampuni ya Twiga ambayo Serikali ni mbia, hivyo naiomba mahakama yako ielekeze upande wa mashtaka kufuatilia na kuona namna ya kufuta shauri hili," alishauri wakili wa utetezi.

Upande wa Jamhuri ulikubaliana na hoja za utetezi na kuahidi kufuatilia suala hilo na kuwasilisha majibu kortini.

Mwanyika na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 39, yakiwamo ya kutakatisha fedha na kukwepa kodi ya Dola za Marekani milioni 112.

Mbali na Mwanyika, washtakiwa wengine ni Meneja Uhusiano wa Mgodi wa Bulyanhulu, Alex Lugendo, Mkurugenzi Mtendaji wa Pongea, North Mara na Bulyanhulu Assa Mwaipopo, Kampuni ya Mgodi ya Pangea, North Mara, Exploration na Bulyanhulu.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza Oktoba 17, 2018.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka matatu ya kula njama, saba ya kughushi, 17 ya utakatishaji wa fedha, kuwasilisha nyaraka za uongo kwa Mamlaka ya Mapato (TRA), kuongoza uhalifu wa kupangwa, manane ya kukwepa kodi na moja la kutoa rushwa.

Washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Aprili 11, 2008 na Juni 30, 2007 katika sehemu tofauti za Jiji la Dar es Salaam, Kahama mkoani Shinyanga, Tarime mkoani Mara na Biharamulo mkoani Kagera, maeneo ambayo yanapatikana ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Prof. Florens Luoga, akionyesha pesa halali na kuwataka wananchi kuwa makini na pesa bandia, alipozungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbunge ahoji kuyeyuka kwa mil. 800/- kodi wawekezaji

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MBUNGE wa Viti Maalum mkoani Shinyanga, Salome Makamba (Chadema), amehoji kuhusu kile anachokiita kuyeyuka kwa Sh. milioni 800, zilizopaswa kulipwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kutoka kwenye viwanda vya wachina ikiwa ni kodi ya huduma.

Makamba alibainisha hayo juzi mjini hapa alipozungumza na waandihi wa habari kuhusu kuendelea kusuasua kwa ukamilishwaji wa ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika manispaa hiyo.

Aliitaja miradi inayosuasua kuwa ni pamoja na wa ujenzi wa machinjio ya kisasa, dampo na kituo cha uwekezaji wa biashara. Alisema kumekuwapo na sintofahamu juu ya ulipwaji wa kodi hiyo ya huduma kutoka kwenye viwanda vya wachina Sh. milioni 800 na alipofuatilia kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga ili kujua hatima ya ulipwaji wa fedha hizo, hakupewa majibu.

"Niliandika barua kwa Mkurugenzi wa Mansipaa ya Shinyanga, ili nipate ufafanuzi juu ya ulipwaji wa kodi ya huduma Sh. milioni 800 kutoka kwenye viwanda vya wachina, pamoja na kusuasua kwa ukamilishwaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ili nione namna ya kusaidia lakini sikupata majibu. "Hivyo, nimeona njia nyingine rahisi ya kupata majibu yangu ni kutumia vyombo vya habari, ndiyo maana nimewaita hapa ili mnisaidie kupata majibu ya maswali yangu kutoka kwa mkurugenzi, juu ya hatima ya ulipwaji wa kodi hii," alisema.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Geofrey Mwangulumbi, alitolea ufafanuzi suala hilo, akieleza kuwa wawekezaji hao hawakupaswa kulipa kodi hiyo kwa sababu bado wana msamaha wa kutolipa kodi hadi mwaka 2023 na wengine 2025. Alisema mradi wa ujenzi wa machinjio ya kisasa uko kwenye hatua ya ukamilishwaji pamoja na wa ujenzi wa dampo la kisasa ambalo wanazungushia ukuta na miradi yote hiyo itakamilika mwezi ujao.

# Simbachawene azuia ukamataji bodaboda

**Na Mwandishi Wetu,**
MPWAPWA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amepiga marufuku ukamataji wa wananchi, bodaboda na kufanya operesheni ya aina yoyote kwa kukurupuka bila kufuata utaratibu, ikieleza kuwa vitendo hivyo vinaweza kusababisha uvunjifu wa amani badala ya kujenga amani.

Ameagiza kila operesheni itakayopangwa kufanywa na Jeshi la Polisi nchini, inapaswa kutolewa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya ili ajue nini kitafanyika kwa kuwa yeye ni Mwenyikiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya.

Akizungumza katika Kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama cha Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma na baadaye kulisisitiza agizo hilo katika Kikao cha Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya jana, Simbachawene alisema ukamataji usio na mpangilio hauna tija na unaweza kuvunja amani badala ya kujenga amani.

"Wananchi wanawalalamikia askari wetu sana kukamata bodaboda bila sababu, siyo bodaboda tu, hata kukamata kamata ovyo watu, ukamataji mwingine unakuwa kama kukomoana, hauna tija, hauleti amani, badala yake unasababisha amani itoweke.

"Yaani msako fulani unatungwa hauna kichwa wala mguu, hauna maelekezo yoyote ya Mkuu wa Jeshi la Polisi au chombo, ni watu tu wanajitungia wanaondoka na pikipiki yao wamepakiana wanaenda kufanya operesheni ambayo haina utaratibu," alionya.

Alisema vyombo vya ulinzi na usalama ni vya wananchi, na operesheni yoyote haipaswi kufanyika bila Mkuu wa Wilaya kupewa taarifa. Ndiyo utaratibu unapaswa kuwa hivyo.

Waziri huyo pia aliupongeza uongozi wa wilaya hiyo kwa kuwa karibu na wananchi kwa kusikiliza kero zao na kuifanya wilaya kuendelea kuwa na amani na utulivu na wananchi kuendelea kuwa na imani na viongozi hao.

"Endeleeni kuwa karibu na wananchi, kwa kusikiliza kero zao na pia kuzitatua, na epukeni malalamiko ya hapa na pale yasiyokuwa ya lazima," alisema.

Simbachawene aliwaomba viongozi wa wilaya hiyo kujipanga vizuri katika maandalizi ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

"Mwaka huu ni wa uchaguzi, wananchi kupitia vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na taasisi zote za utawala, mnapaswa kuwa na ushirikiano mkubwa ili kujenga msingi wa uchaguzi utakaokuwa wa amani na utulivu," alisema.

Alisema mwaka wa uchaguzi haupaswi kuwa na vurugu, bali kuwa na utulivu ili kukuza demokrasia.

"Rai yangu kwa wananchi, kuhakikisha kwamba tunapaswa kujenga utulivu kuanzia sasa kuelekea uchaguzi mkuu, hatupaswi kuwa na vurugu, ni mwaka ambao amani na utu-

# DPP aagiza mahabusi 85 waachiwe huru

**Na John Mapepele,**
SINGIDA

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, ameagiza mahabusi 85 katika Gereza la Wilaya ya Manyoni mkoani Singida waachiwe huru baada ya kukiri kufanya makosa mbalimbali.

Mganga alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea gereza hilo katika ziara yake mkoani Singida, yenye lengo la kuzindua Jukwaa la Haki Jinai.

Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Rehema Nchimbi, alizindua jukwaa hilo jana, huku DPP Mganga akisema linalenga kupambana na uhalifu wa kijinai katika mikoa yote nchini na hivyo kupunguza mrundikano wa mahabusi.

Dk. Nchimbi alisema kuzinduliwa kwa jukwaa hilo kutakuwa nguzo kuu ya kuzima uhalifu katika Mkoa wa Singida na kuwataka wajumbe kutumia jukwaa hilo kufanya utatifi na kutafakari kwa kina namna bora ya kudhibiti uhalifu badala ya kusubiri utokee na kupeleka kesi mahakamani.

"Kama kwenye mambo mengine tumeweza kushika nafasi ya kwanza kitaifa, kwanini tusiwe wa kwanza kufanya kazi nzuri kwenye kutekeleza majukumu ya Jukwaa la Haki Jinai kwenye mkoa wetu na wengine waje kujifunza kwetu? Inawezekana endapo kila mtu atatekeleza wajibu wake," alisema.

Dk. Nchimbi alisema hata vitabu vitakatifu vinasema 'mwisho wa uhalifu ni mbaya na msharaha wa dhambi ni mauti', akieleza kila ofisi na idara ya serikali katika Mkoa wa Singida kuwa na mfumo wa Jukwaa la Haki Jinai ambao utasaidia kujenga mfumo wa kutafakari na kudhibiti uhalifu badala ya kusubiri utokee.

Kwa upande wake Mganga alisema kwa mujibu wa Sheria ya Mashtaka ya mwaka 2008 Ibara ya 59(B)(II), ana jukumu la kuratibu upelelezi wa kesi zote za jinai nchini japokuwa anaweza kukasimu madaraka hayo kwa vyombo vingine vya serikali.

Alisema ofisi yake imedhamiria kutokomeza uhalifu wa kijinai kwa kutekeleza mkakati wa kuunda kwa majukwaa hayo nchini.

Mganga alisema kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo na ongezeko wa uhalifu wa kijinai, serikali iliamua kufanya marekebisho makubwa ya kupambana na tatizo hilo kwa kuunda Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kutangaza kwenye Gazeti la Serikali namba 49, la Februari 13, 2018 tofauti na awali ambapo Kurugenzi ya Mashtaka (DPP) ilikuwa chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.



Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani, Jokate Mwegelo (kulia), akipokea msaada wa mifuko ya saruji 300 kutoka kwa Mkurugenzi wa Masoko na Ukuzaji wa Biashara wa Benki ya TPB, Deo Kweyuka, kwaajili ya ujenzi wa mabweni ya wasichana, katika hafla iliyofanyika wilayani Kisarawe, mkoani Pwani juzi. Kushoto ni Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa Benki hiyo, Chichi Banda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Mwanri asisitiza bajeti ya 1,000/- kwa kila mtoto

**Na Tiganya Vincent,**
TABORA MJINI

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, amesema hatapitisha bajeti ya halmashauri itakayoshindwa kutenga Sh. 1,000/- kwa ajili ya kila mtoto aliye chini ya miaka mitano kama ilivyoagizwa.

Amesema kila halmashauri inatakiwa kupitia mapato yake ya ndani, itenge kiasi hicho cha fedha kila mwaka kulingana na idadi ya watoto walioko katika eneo lake. Mwanri alitoa kauli hiyo jana wakati akifungua kikao cha tathmini ya nusu mwaka ya mkataba wa lishe ngazi ya mkoa.

Alisema katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha, ni vyema kila halmashauri ihakikishe imetenga fedha hizo ili kukidhi matakwa ya mapambano dhidi ya utapiamlo. Mwanri alisisitiza kuwa halmashauri ambayo haitaweka wazi mipango yake, haitapita wakati wa Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha kupitia bajeti.

Mkuu wa Mkoa huyo alisema masuala ya lishe lazima yawe ajenda ya kudumu ya kuanzia ngazi za vijiji hadi mkoa na kwenye nyumba za ibada.

Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, alisema asilimia 25.8 ya watoto mkoani humo wamedumaa na hawafundishiki ili kuleta tija katika uchumi wa taifa.

Aliwataka maofisa wanaohusika na mipango na bajeti, kuhakikisha wanashirikiana na makatibu wa afya na maofisa lishe kupanga mipango lishe kwenye bajeti.

## TCRA yaikuna Kamati Amani

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Amani Mkoa wa Mbeya imeipongeza Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) kwa kutoa elimu juu ya utumiaji wa huduma za mawasiliano na kujikinga na uhalifu unaofanyika kwa huduma hizo.

TCRA iko katika Kampeni ya 'Sirubuniki kuwa Mjanja', ambayo imeanza mkoani Mbeya na kuzunguka nchi nzima kwa lengo la kutoa elimu hiyo kwa jamii.

Akizungumza jana katika kampeni hiyo na viongozi wa dini, Mkuu wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wa TCRA, Asajile John, alisema viongozi ni watu muhimu katika kutoa elimu kwa waumini wao pamoja na jamii kwa ujumla.

Alisema huduma ya mawasiliano ni pana na teknolojia inabadilika kila siku, hivyo TCRA itaendelea kutoa elimu kuhusiana na matumizi ya mawasiliano na kuhakikisha yanakuwa salama kwa ustawi wa nchi.

Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa TCRA, Mabel Masasi, alisema katika kampeni hiyo wanayafikia makundi yote na kuhakikisha yanapata elimu juu ya matumizi sahihi ya mawasiliano na kuepukana na matatizo ya kihalifu yanayoweza kutokea.

"Wakati umefikia wa kutumia mawasiliano kwa kulinda usalama wa nchi, na watu ambao wanatumia mawasiliano vibaya mkono wa sheria utawakuta popote walipo na ndiyo maana tumeanzisha kampeni hii ili kutoa elimu ya watu kuepukana na mkono wa sheria," alisema.

Askofu Msaidizi wa Kanisa la Anglican Mbeya, Daudi Sichinga, alisema umefika wakati viongozi wa dini kushikamana kwa pamoja na TCRA kwa ajili ya kutoa elimu hiyo kwa kuwa sekta ya mawasiliano inakua kwa kasi.

Alisema elimu ambayo ameipata ataipeleka kwa waumini wake ili kuepukana na kesi zisizo na msingi na kujikinga na uhalifu unaotumika kwa njia ya mawasiliano na badala yake kujenga ustawi wa nchi.

"Tunapongeza hatua ya TCRA kuona umuhimu wa kuanzisha kampeni hii na tutashirikiana kwa pamoja na pia nashauri taasisi nyingine kuiga mfano wa TCRA katika kuelimisha umma kwani viongozi wa dini wana wafuasi wengi na ushawishi mkubwa katika jamii," alisema.

Sheikh wa Wilaya ya Mbeya, Abdallah Omar, alisema kampeni hiyo ya TCRA wanayoshirikiana na Jeshi la Polisi, itakuwa chachu ya mabadiliko kwa jamii kwa kuwa wengi wanajikuta kwenye matatizo kwa kukosa uelewa wa matumizi ya mawasiliano.

"Kumekuwa na matukio mengi ya uhalifu unaofanyika kwa njia ya mawasiliano, kampeni hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kwa jamii jinsi ya kujikinga ili wasirubuniwe wanapotumia huduma za mawasiliano," alipongeza.



Wakazi wa Kata ya Kiriba, wilayani Musoma, mkoani Mara, wakishiriki katika kazi ya kusomba mawe juzi, kwa ajili ya ujenzi wa msingi wa madarasa ya Shule ya Sekondari Kiriba. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Simbachawene ataja mwarobaini kupunguza mahabusi magerezani

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amelitaka Jeshi la Polisi kuangalia aina ya makosa ya watuhumiwa ambayo yanadhaminika ili kupunguza mlundikano wa mahabusi magerezani.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua miradi ya maendeleo ya Jeshi la Magereza na baadaye kuzungumza na maofisa na askari wa Makao Makuu ya Jeshi hilo, jijini Dodoma jana, Simbachawene alisema jeshi hilo linakabiliwa na changamoto ya idadi kubwa ya mahabusi kulinganisha na wafungwa waliokо magerezani.

"Mlundikano wa mahabusi magerezani ni changamoto kubwa lakini inapaswa kuangaliwa kwa upana zaidi hasa kwa Jeshi la Polisi kuangalia makosa yanayodhaminika ili wasizalishe mahabusi kwa sababu zisizo za msingi," alisema Simbachawene.

Kwa kufanya hivyo, alisema kutasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano magerezani sambamba na kuipunguzia serikali gharama ya kuwahudumia wafungwa na mahabusi.

"Tunajaza magereza yetu kwa kuzalisha mahabusi kwa makosa ambayo mengine hayastahili kuwaleta magerezani kama vile ugomvi wa kifamilia na makosa mengine madogo madogo ambayo yanadhaminika," alisisitiza Simbachawene.

Aidha, akitoa taarifa ya jeshi hilo, Kamishna Jenerali wa Magereza (CGP), Suleiman Mzee, alisema kwa sasa kuna wafungwa 14,502 na mahabusi 17,396 katika magereza yote nchini.

"Tutajitahidi kuendelea kushirikiana kwa pamoja katika jukwaa letu la haki jinai ili kuangalia namna bora ya kutatua tatizo au changamoto ya msongamano wa mahabusi magerezani," alisema Kamishna Jenerali Mzee.

Mzee alimshukuru Waziri Simbachawene kwa kufanya ziara Makao Makuu ya Magereza na kuahidi kuyafanyia kazi maagizo mbalimbali aliyoyatoa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

# Ufaransa yamwaga bil. 3/- kukuza kilimo hai Afrika

**Na Faustine Feliciane,** ZANZIBAR

UFARANSA kupitia Shirika lake la Maendeleo (AFD) imetoa Euro milioni 1.49 (zaidi ya Sh. bilioni tatu) kufadhili shughuli za kilimo hai kwa Tanzania, Uganda na Morocco.

Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 90 ya Euro milioni 1.6 zilizotolewa na wafadhili mbalimbali ili kuhamasisha kilimo hai kwenye nchi hizo.

Akizindua jana Mradi wa Ubunifu wa Kitaasisi kuhusu Kilimo Hai, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko wa Zanzibar, Balozi Amina Salum Ali, alisema kwa kutambua umuhimu wa kilimo hai kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko kwenye mchakato wa kutengeneza sera zitakazokitambua kilimo hai.

Balozi Amina alisema mradi huo ni muhimu kwa kuendeleza kilimo hai visiwani hapa huku akitanabaisha kwamba watazingatia mnyororo wa thamani kuanzia maandalizi ya shamba hadi kumfikia mlaji kwa kuwa na mazao ya viwango bora ili kukamata soko kimataifa.

"Zanzibar tunatambua umuhimu wa Kilimo hai. Kwa kutambua suala hilo, kwa sasa tunatayarisha sera zitakazoshughulikia masuala yote ya kilimo hai lakini pia tutakuwa na kituo cha viungo na mafuta ya majani asilia. Haya mazao yanazalishwa kwa wingi hapa Zanzibar. Lengo ni wakulima wetu wadogo ambao wengi ni wanawake, kupata soko na kufanya kilimo kisicho na gharama chenye kutunza mazingira.

"Uzinduzi huu umekutanisha wataalam wa kilimo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia tunao wabunge na kila mtu hapa amekiri kuunga mkono kilimo hai na manufaa yake.

"Kilichopo sasa ni Tanzania kufanya kilimo hiki ili kukamata soko la mazao hai yenye fursa ya mabilioni ya fedha nje ya nchi na wananchi wakila vyakula bora vyeye kulinda afya zao dhidi ya maradhi yasiyoambukizwa," alisema Balozi Amina. Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, alisema nchi yake itaendelea kusaidia Tanzania katika kilimo hai kuhakikisha inakuwa mfano katika uzalishaji wa mazao pasipo kutumia kemikali.

Alisema mwaka 2021 wanatarajia kuingiza rasmi Zanzibar kwenye miradi ya kuendeleza kilimo hai na kuongeza ufadhili ikiwamo kuwajengea uwezo wakulima kwa maendeleo endelevu. "Tanzania inaendelea kupiga hatua kubwa kwenye kilimo hai. Tunaamini nchi hii itakuwa kituo kikubwa cha kilimo hai lakini ni wazi kilimo hai kinakabiliwa na changamoto za mabadiliko ya tabianchi na kutunza mazingira. Kinawezesha Watanzania kukamata soko la dunia katika mazao mbalimbali," alisisitiza Balozi Clavier.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mahmoud Mgimwa, aliahidi kupeleka mjadala wa kilimo hai bungeni ili kitengewe bajeti wakati wa mjadala wa bajeti ya kilimo kwenye kikao kijacho cha Bunge.

# Mbeya kinara mimba utotoni

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umetajwa miongoni mwa mikoa saba yenye kiwango kikubwa cha mimba za utotoni.

Hayo yalisema jana na Mkuu wa Ofisi ya Shirika la Umoja wa mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef), mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Pamela Shao, wakati wa uzinduzi wa mtandao wa vijana Afrika, Tawi la Mbeya na Songwe, unaofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Taifa linaloshughulika na Idadi ya Watu (UNFPA).

Shao alisema Mkoa wa Mbeya una asilimia 33 ya mabinti wenye umri kati ya miaka 15 na 19 ambao wameshapata watoto ikizidi asilimia 21 ya kitaifa.

Shao alisema miongoni mwa sababu zinazochangia ongezeko hilo la mimba za utotoni ni maisha ya vijana wa Tanzania ambao wako katika kundi rika la balehe kubadilika hususani wasichana wanaoishi kwenye mazingira magumu.

"Licha ya Mkoa wa Mbeya kuwa kinara wa mimba za utoto pia ni ya mikoa mitatu kitaifa kwa kuwa na maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU) na kundi kubwa la waathirika ni mabinti," alisema Shao.

Alisema Unicef kwa kushirikiana na serikali, imeendelea na program mbalimbali za elimu ili kuwaelimisha mabinti juu ya maambukizi mapya ya VVU ikiwamo programu ya rika balehe na lishe.

Msimamizi wa Mradi wa Mtandao wa Vijana Afrika, Jaquiline Mahone, ambaye ni Mwakilishi Mkazi wa UNFPA, alisema moja ya mikakati ni kuishauri serikali kuboresha huduma za afya ya uzazi.

Mahone alisema suala la afya ni mtambuka lakini wao watajikita katika kutoa elimu ya afya ya uzazi juu ya kukabiliana na maambukizi mapya ya VVU.


Alisema uzinduzi wa mtandao wa vijana Afrika (AfriYAN) Tawi la Mbeya na Songwe utakuwa na manufaa kwa sababu utawafikia vijana wengi ili kuongeza ujuzi na maarifa kwenye masuala mtambuka ikiwamo afya na elimu.

Mgeni rasmi katika ufunguzi huo, Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, aliwataka vijana kujitambua na kuamua hatima ya maisha yao bila kufuata mikumbo.

Alisema miongoni mwa sababu zinazochangia vijana kushindwa kufikia ndoto zao ni kuwa na haraka ya maisha mazuri badala ya kuwa wavumilivu katika kutafuta.

"Vijana hupenda kukimbizana na maendeleo bila kuwa na mipangilio madhubuti na miongoni mwa sababu zinazochangia na kuwasiliza mara kwa mara wachochea mada za fursa na kusahau kufuata misingi na malengo yao waliyojiwekea," alisema Dk. Tulia.

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# Mungu ibariki Serengeti Girls michuano ya dunia

**SAFARI** ya Tanzania kuwania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia kwa wasichana wa umri chini ya miaka 17 inatarajia kuendelea tena kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Wenyeji Timu ya Taifa ya vijana ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls)itawakaribisha wapinzani wao Uganda katika mchezo wa kwanza wa raundi ya pili ya michuano hiyo.

Tanzania imefika hatua ya pili baada ya kuwaondoa Burundi kwa jumla ya mabao 6-1 wakati Uganda yenyewe iliwafunga Ethiopia magoli 5-1, timu zote mbili zikimalizia ugenini Bujumbura na Addis Ababa.

Kuelekea mchezo huo, Shirikisho la Soka (TFF), limeendelea kuwaita mashabiki kutoka sehemu mbalimbali jijini Dar es Salaam na mikoa ya jirani kujitokeza kwa wingi kuwashangilia mabinti zao ambao wanahitaji kupata matokeo chanya katika mchezo huo wa kwanza.

Matokeo chanya ndiyo yataipa wepesi Serengeti Girls katika mchezo wake wa marudiano ambao utachezwa Kampala baada ya wiki moja.

Ushindi wa aina yoyote utawafanya binti hao kuwa na kibarua chepesi ugenini na kuendeleza rekodi nzuri ya ushindi waliyoianza katika michuano hiyo na hatimaye ndoto ya Tanzania kushiriki fainali za Kombe la Dunia zikatimia.

Ni wazi na tunaamini shabiki ni mchezaji wa 12 uwanjani, tunatakiwa tujitokeze kwa wingi kwenda kuwashangilia mabinti hawa ambao hapo baadaye watapeperusha bendera ya nchi katika kikosi cha Twiga Stars.

Mashabiki wanatakiwa kuitendea haki timu hii ikiwa nyumbani kwa kufika uwanjani kuwashangilia na kudhihirisha wako kwenye ardhi yao kwa kuwaunga mkono kuanzia dakika ya kwanza hadi filimbi ya mwisho ya mchezo huo muhimu.

Historia inaweza kuandikwa kwa Watanzania kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia kupitia wasichana au wanawake, hivyo gazeti hili linawaomba wadau wote wa michezo kujitokeza kuwashangilia mabinti hawa ili wafanye vema kama walivyofanikiwa kupeperusha vizuri bendera ya nchi katika mashindano ya Kombe la Chalenji yaliyofanyika Jinja, Uganda kwa kushirikisha timu sita za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Hakuna kisichowezekana, kama nchi nyingine zilipata mafanikio, hata Tanzania inaweza kung'ara katika mashindano ya mwaka huu na kufungua ukurasa mpya wa kutangaza vipaji vya wachezaji wa hapa nchini.

Licha ya kufanya vizuri katika mechi zilizopita, bado Nipashe linawakumbusha wachezaji wa Tanzania kucheza kwa kiwango cha juu na kutobweteka na matokeo ya mechi zilizopita.

Tunawaombea vijana wetu washuke dimbani wakifahamu Watanzania wanahitaji kupata ushindi na hatimaye kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kusonga mbele, huku wakifahamu watakuwa na kibarua kizito watakapokwenda kumalizia dakika 90 za ugenini huko Kampala.

Huu ni wakati muhimu kwa utawala wa Rais, Wallace Karia, kuhakikisha wanatimiza malengo yao ya kuipeleka nchi katika fainali hizo na kuuondoa msamiati wa 'Tanzania ni kichwa cha mwenzawazimu' kwa kufuzu fainali hizo.

Kama Taifa Stars ilifanikiwa kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika zilizopita, tunaamini pia Serengeti Girls wanaweza kuiletea furaha nchi katika kampeni hii ya kuelekea India kwenye fainali za dunia.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki kikosi chetu cha Serengeti Girls.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Muhimu kwa wacheza kandanda

**MPIRA** ni kitu cha mviringo kilichotengenezwa kwa ngozi kwa ajili ya michezo; mchezo unaotumia kifaa kilichotengenezwa kwa mpira. Mpira wa miguu una majina mengi: kandanda, kabumbu, soka. Mingine ni mpira wa pete, mpira wa wavu na mpira wa magongo.

Maana ya pili ya 'mpira' ni mti mkubwa kiasi wenye majani mapana yaliyogawanyika unaotoa utomvu unaotengeneza vitu vya mpira.

Zamani, kandanda ulikuwa mchezo wa kuwapa mazoezi wachezaji na wakati huohuo kuwaburudisha watazamaji. Wachezaji hawakulipwa hela kwani watazamaji waliingia viwanjani bure kufurahia mchezo huo.

Sasa mambo ni tofauti kwani mchezo wa kabumbu ni kazi na wachezaji hulipwa mishahara, tena mikubwa kuliko hata wanaofanya kazi walizosomea! Naam, "kila zama na kitabu chake," chambilecho wazungu.

Kuna methali isemayo "Kipendacho moyo ni dawa" kwamba kitu anachokipenda mtu au inachokipenda roho ya mtu huwa ni kama dawa yake. Methali hii hutumiwa kumpigia mfano mtu anayeelekea kukipenda kitu fulani sana ingawa wengine wanakiona kuwa cha kawaida au kibaya.

Hata kwenye kabumbu kuna baadhi ya wachezaji mahiri wanaovipenda mno vilabu vyao kiasi cha kutotaka kujitafutia hela zaidi kwenye vilabu vingine, ndani au nje ya nchi. Labda baadhi yao huogopa kwenda nje ya nchi kwa kutojua lugha ngeni. Hawapaswi kuogopa kwani tatizo hilo waiachie miguu yao ndiyo itakayozungumza.

Masilahi hayo ni mishahara itakayokubaliwa na pande zote mbili, kulipwa kwa wakati kwa kuwekewa kwenye akaunti zao za benki bila ubabaishaji kama ilivyo sasa. Ili kutimiza masharti hayo, wachezaji wawe na chama chao kitakachoendeshwa na wachezaji wastaafu kwani ndiwo wanaojua matatizo na stahiki za wachezaji. Kuwe na mwanasheria atakayesimamia mikataba ya wachezaji na vilabu.

Katika mikataba hiyo kuwe na kigezo (kielelezo, kipimo maalumu cha kufuatwa; sheria inayoongoza kutolewa uamuzi) kinachowapa wachezaji uhuru wa kujiunga na vilabu vingine vitakavyowapa masilahi mazuri zaidi. Mchezaji atakayeitumikia klabu yake kwa bidii, nidhamu na mafanikio apewe tuzo ya aina fulani na ikiwezekana aongezwe mshahara.

Atakayefanya kinyume, kama kutokuwa na nidhamu uwanjani kwa kuoneshwa kadi iwe ya njano au nyekundu mara kwa mara, ama nje ya uwanja kwa kushiriki ulevi, uvutaji sigara, dawa za kuongeza nguvu, uasherati n.k. apewe onyo la kwanza na akiendelea apewe la pili na la tatu afukuzwe na kulipwa masilahi yake yote.

Kadhalika mchezaji asilazimishwe kushiriki vitendo vya ushirikina iwe ndani, nnje au viwanjani. Kama hataki kwa sababu ya kumwamini Mungu wake, asichukiwe wala kuadhibiwa kwa kukomolewa (kumfanyia tendo la kumsumbua au kumuumiza) kwa namna moja au nyingine. Awe huru kukubali au kukataa, kwa mujibu wa imani yake.

Aidha vilabu viwekewe masharti ya matumizi ya fedha kwamba kila kinachonunuliwa kiwe na risiti inayothibitisha ununuzi. Kwa ufupi, kila hela inayotoka klabuni iwe kwenye maandishi na ukaguzi ufanywe na wakaguzi wasiokuwa na tamaa ya hela ili wafanye kazi yao kwa haki bila ghiliba (udanganyifu wenye nia ya kujinufaisha).

Wahenga hunishangaza sana kwa methali zao. Kwa mfano walisema: "Mtaka cha mvunguni sharti ainame." Maana yake anayekitaka kitu kilicho mvunguni mwa kitanda lazima ainame ndipo aweze kukichukua. Hii ni methali ya kutukumbusha kwamba tukitakapo kitu lazima tuwe tayari kukifanyia kazi au kukisumbukia. Kumbe ndo maana chaguzi zote husumbukiwa kwa hali na mali usiku na mchana!

Vilevile vilabu vyapaswa kuwakumbuka wachezaji wao waliostaafu wanapopata maradhi hata kutoweza kujitibu. Kuna wachezaji wengi wa vilabu vikubwa nchini, hasa vya Simba na Yanga walioviletea vilabu hivyo sifa kubwa ndani na nnje ya nchi lakini sasa hawathaminiwi wala kukumbukwa! Au ndio kile kisemwacho "Yaliyopita si ndwele ganga yajayo"?

"Asante tupu haijazi chungu." Shukrani au asante isiyo na kitu haijazi chungu. Tuwafariji waliofikwa na maafa fulani kwa vitendo wala sio maneno matupu tu.

**marobarnabas@yahoo.com 0784 334 096**

HABARI KITAIFA

# Fursa soko la mboga, matunda zaibuka Ulaya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI 15 zinazohusisha wazalishaji na wasafirishaji wa bidhaa za mboga na matunda zimejiongezea fursa katika soko la Ulaya.

Fursa hiyi imetokana na ushiriki wao katika Maonyesho ya Kimataifa ya Mboga na Matunda yajulikanayo kama 'Fruit Logistica 2020' yaliyofanyika Februari 5 hadi 7, mwaka huu, Berlin nchini Ujerumani.

Mazao yaliyovutia wanunuzi na wadau wengine katika maonyesho hayo ni maparachichi, rasiberi, pasheni, ndimu zisizo na mbegu, njegere, 'snow peas na sugar snaps, maharage machanga (green beans), 'french Beans, babycarrots, aina mbalimbali za jamii ya pilipili, viungo vya chakula kama vile tangawizi, nana (mint), kitunguu jani (chives), matikiti maji na mafuta ya parachichi.

Taarifa iliyotolewa nchini na Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, Balozi Dk. Abdallah Possi, ilisema mafanikio ya ushiriki wa Tanzania yamekuwa makubwa kutokana na makubaliano ya kimkakati yaliyofikiwa baina ya wafanyabiashara wa Tanzania na wanunuzi wa mbogamboga na matunda wa nchi za Ulaya.

Balozi Possi alinukuliwa katika taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) kuwa hali imeleta viashiria chanya vya kupata masoko makubwa. Makubaliano hayo yanatarajiwa kuimarisha biashara kati ya Tanzania na nchi za Ulaya, hivyo kuvutia uwekezaji katika sekta husika nchini.

Alisema wafanyabiashara wamekutana na kuingia makubaliano na wanunuzi, wabia wa biashara na wadau muhimu kama vile Kituo cha Biashara cha Kimataifa (ITC) na Taasisi ya Kimataifa ya GLOBALG.A.P inayoshughulikia viwango vya ubora wa bidhaa za kilimo na mifugo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, taasisi hizo ni wadau muhimu katika kuwawezesha wazalishaji kutumia njia salama, sahihi na endelevu katika uzalishaji na kuwaunganisha na masoko ya kikanda na kimataifa.

Sambamba na hilo, taarifa ilisema washiriki walijifunza teknolojia za kuzalisha, kusindika, kufungasha, kuhifadhi na kusafirisha mazao ya kilimo ili kukidhi mahitaji ya soko la Ulaya.

"Binafsi nilikutana na mzalishaji kutoka Tanzania ambaye ameingia makubaliano na mwekezaji kutoka Ujerumani. Hii inamaanisha maonyesho haya pia yalikuwa fursa kwa wazalishaji wa Tanzania kutafuta wabia wa biashara," alisema Balozi Possi.

Alisema mkakati wa ubalozi ni kuandaa na kuratibu matukio maalum kama vile maonyesho, semina na mikutano ya ana kwa ana ya wafanyabiashara ili kuwakutanisha wafanyabiashara wa Tanzania na wadau muhimu wa nchi za Ulaya.

Pia alisema Ubalozi wa Tanzania ulioko Berlin umekuwa ukihimiza ushiriki wa Tanzania katika maonyesho yanayofanyika nchini humo ili kutafuta fursa zaidi za kibiashara.




Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoa wa Singida, Edson Mwakihaba (kushoto) na Meneja Uhusiano na Serikali wa kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Neema Temba (kulia), wakikabidhi makoti ya usalama barabarani kwa Mwenyekiti wa bodaboda wa Singida Mjini, Abdul Misigo, katika hafla ya kampeni ya SBL 'Usinywe na kuendesha chombo cha moto', iliyofanyika katika Stendi ya mabasi ya mkoa huo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri tengeni ardhi ya kilimo kwa vijana - Mgumba

**Na Mwandishi Wetu,**
NJOMBE

NAIBU Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, ameziagiza halmashauri zote nchini kutenga ardhi ya kutosha kwa ajili ya vijana kuzalisha mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Alitoa agizo hilo jana mjini Njombe alipofungua kongamano la vijana wa mikoa ya Njombe, Ruvuma na Iringa kujadili fursa zilizoko katika sekta ya kilimo nchini.

Mgumba alisema kumekuwapo malalamiko ya vijana kukosa ardhi kutokana na halmashauri kuwa na mashamba pori mengi yasiyopimwa na kulimwa.

"Halmashauri zote zihakiki mashamba pori yote au yaliyochukuliwa mikopo na hayalimwi yapimwe na kugawiwa kwa vijana walio tayari kufanya kazi za kilimo nchini," aliagiza.

Ili kufanikisha hilo, Mgumba aliwataka vijana kujisajili kwenye daftari la wakulima linaroratibiwa na wizara yake ili serikali iwatambue na kujua vikwazo vinavyowakabili kisha kuwaonyesha fursa za ajira kwenye kilimo.

Mgumba alisisitiza halmashauri kutoa fedha za mikopo kwa vijana bila urasimu ili vijana wanufaike na kuanzisha kazi za uzalishaji mazao ya kilimo na mifugo.

Alisema serikali imeelekeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kuendelea kutoa mikopo kwa vijana ili wapate mitaji.

"Wapo vijana wengi wasomi wameamua kujiajiri katika kilimo ili kufikia malengo ya kuongeza ajira ikiwa ni malengo ya serikali ya awamu ya tano kukuza sekta ya kilimo," alisema.

Alisema Tanzania ina eneo la hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo, hivyo vijana wajitokeze kutumia fursa hiyo kuanzisha kazi za kuzalisha mazao ya kilimo.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Ruth Msafiri, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Njombe, aliziagiza halmashauri zote za mkoa huo kuandaa katiba kwa ajili vijana kushiriki shughuli za kilimo.

Aliongeza kuwa watendaji wote wa halmashauri wapunguze urasimu kwa kukaa muda mrefu bila kupitisha maombi ya vijana wanaostahili mikopo ya fedha za mapato ya ndani.

"Halmashauri punguzeni urasimu, msikae zaidi ya robo mwaka bila kutoa mikopo kwa vijana, kinamama na walemavu," aliagiza.

Kongamano hilo la siku mbili linawakutanisha vijana wapatao 200 kutoka mikoa ya Njombe, Ruvuma na Iringa chini ya uratibu wa Wizara ya Kilimo na wadau toka wizara za kisekta na taasisi binafsi.

# Uhaba madarasa wakumba Kigoma

**Na Pendo Thomas,**
KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali (mstaafu) Emmanuel Maganga, amesema mkoa unakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo katika shule za sekondari na za msingi.

Maganga aliyabainisha hayo jana wakati Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Kigoma kilipowasilisha mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya kuchangia uboreshaji miundombinu ya elimu

Alisema mkoa una upungufu wa vyumba vya madarasa 397 kutokana na uhitaji wa vyumba 1,953 wakati vilivyopo ni 1,556 hivyo msaada huo utasaidia katika ujenzi na kupunguza upungufu huo.

"Nitoe wito kwa vyama na taasisi zingine zilizoko mkoani Kigoma kuiga mfano wenu kuchangia maendeleo. Nawaomba pia wenyeji wa Kigoma kurudisha fadhila ili vijana waendelee kusoma," alisema.

Pia Maganga alisema kutokana na upungufu huo, wanafunzi wengine wanalazimika kusomea kwenye vyumba vya maabara na wengine katika mabwalo ya chakula wakati taratibu za kutatua changamoto hiyo zikiendelea.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji, Mwailwa Pangani, alisema manispaa ina upungufu wa vyumba vya madarasa 38 katika shule za sekondari, Shule ya Sekondari ya Gungu pekee ikiwa na uhitaji wa vyumba tisa.

Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Kigoma, Martin Mpemba, alisema kulingana na kutambua uhitaji wa vyumba vya madarasa, wameamua kutoa msaada huo.

Mpemba alisema wakiwa wadau muhimu wa elimu, wameona wawe mfano kusaidia uboreshaji wa sekta hiyo pamoja na kuahidi kuendelea kuweka mipango mbalimbali ya kuchangia kumaliza upungufu wa vyumba vya madarasa mkoani Kigoma.

# Waomba ajira kwa wataalamu mionzi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imeombwa kuajiri wafanyakazi wa fani ya mionzi ili kuondokana na kutumia watu wasio na taaluma hiyo.

Ombi hilo lilitolewa na Rais wa Chama cha Watu wa Mionzi na Tiba nchini (TARA), Stephen Mkolama, katika kongamano la sayansi lililofanyika jijini hapa huku akisema hali hiyo itapunguza msongamano na kuzidiwa kwa waliopo.

Alisema watumishi wa fani hiyo wanafanya kazi ngumu kutokana uhaba wa watu wenye taaluma waliopo katika kitengo cha mionzi.

Mkolama alisema mionzi ni kitengo muhimu kinahitajika kuwa na wafanyakazi wengi ili kurahisisha utendaji kazi.

"Tunaomba serikali iliangalie hilo. Hiki ni kitengo muhinu na kinahitaji watu waliosomea taaluma hiyo. Kinachotakiwa ni kuona watu wa mionzi wanaangaliwa vizuri ili wafanye kazi yao kwa ufanisi," alisema.

Rais huyo alifafanua kuwa lengo lao ni kuona kitengo hicho kinakuwa imara na kuangaliwa kwa ukaribu ili kifanye kazi kwa ufasaha zaidi.

Naye, Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Eliud Eliahakimu, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye kongamano hilo, alisema serikali iko pamoja nao, hivyo kuwataka kufanya kazi kwa ufasaha.

Alisema maombi yao ameyachukua na kuwataka kuendelea kufanya kazi kama kawaida wakati wakisubiri uamuzi utolewe.

"Nawaomba tuendelee kujituma, kitengo mlichopo ni cha muhimu na kinahitaji kufanyiwa kazi. Mionzi ni tiba muhimu, hivyo ni vyema mkafanya kazi kwa malengo ili kutoa taarifa nzuri," alisema.

Aliongeza kuwa serikali inakitambua kitengo hicho pamoja na umuhimu wake katika tiba za mionzi ambazo wanazitoa, hivyo itakuwa mstari wa mbele kufanyia kazi maombi hayo.

# JKT sasa wakwepa kuitwa ombaomba

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Brigedia Jenerali, Charles Mbuge, ameanza kufanyia kazi maagizo ya Rais John Magufuli ya kuifanya SumaJKT ijitegemee badala ya kuwa ombaomba.

Utekelezaji wa maagizo hayo ulianza kujidhihirisha jana alipotangaza jijini Dar es Salaam kupokea malori manne na pikipiki tano zilizonunuliwa kwa fedha zitokanazo na mapato ya ndani ya jeshi hilo.

Ununuzi wa malori na pikipiki hizo umefanywa kwa gharama ya Sh. milioni 469, ikiwa ni utekelezaji wa maagizo yake aliyotoa mara baada ya uteuzi wake Septemba mwaka jana.

Akizungumza kabla ya kupokea malori na pikipiki hizo, Brigedia Jenerali Mbuge ambaye pia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Uzalishaji Mali (SumaJKT), alisema magari hayo yana thamani ya Sh. milioni 457.1 na pikipiki Sh. milioni 12.2 na yametokana na fedha za ndani.

"Hatua hii tuliyofikia ya kuanza kununua vyombo vya usafiri na usafirishaji itawezesha shirika letu la SumaJKT kufikia malengo yake ikiwamo ununuzi wa magari ya kusindikiza fedha na kuanzisha Chuo cha Ulinzi Binafsi.

"Chuo hiki kitatoa mafunzo kwa vijana waliopitia JKT kwa kuwafundisha ulinzi wa majengo. Hii itasaidia uendeshaji wa malezi ya vijana na kukuza uchumi wetu wa ndani," alisema.

Aliongeza kuwa jitihada zinazofanywa kwa kutumia vyanzo vya ndani na kuanzisha miradi kwa asilimia 100 ni juhudi zinazoonyesha shirika linakua.

Aliwapongeza watendaji wote wa Suma Guard na SumaJKT kwa kazi nzuri wanazofanya siku hadi siku na matunda yameanza kuonekana.

Brigedia Jenerali Mbuge alisema shirika hilo kupitia Suma Guard lilianzishwa mwaka 2010 likiwa na walinzi saba Mkoa wa Dar es Salaam na sasa wamefikia 10,633 nchi nzima walioko katika maeneo 441 ya kazi.

"Hii imechangia shirika kufanya shughuli za kiulinzi na kujitegemea na leo (jana) tunashuhudia ununuzi wa magari na pikipiki, taasisi za serikali na watu binafsi watumieni walinzi wa Suma Guard ili kusaidia serikali kupunguza tatizo la ajira,"alisema.

Kiongozi huyo alisema shirika hilo limekuwa likitoa ajira kwa vijana hao ili wasirudi mtaani na kuiga tabia ambazo hawakufundishwa ndani ya jeshi.

Brigedia Jenerali Mbuge alimshukuru aliyekuwa Mkuu wa Kikosi cha Itende Mbeya 844 kwa juhud zake za kushirikiana na maofisa kununua lori moja.

Mkurugenzi Mtendaji wa SumaJKT, Kanali Rajab Mabele, alisema wako katika mchakato mwingine wa kupata magari mengine sita ya tani 18.

"Tunafanya taratibu hizi kupitia Benki ya CRDB, mchakato upo sehemu nzuri. Nikuhakikishe Brigedia Jenerali Mbuge kama ulivyotuagiza mara baada ya kuteuliwa kwako, tunaendelea na utekelezaji, tutanunua pia na mitambo," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya SumaJKT, Meja Jenerali mstaafu Farrah Mohammed, alisema tangu alipoingia katika jeshi hilo mwaka jana, amelifanya shirika hilo kuwa la kisasa kwa kuwa na mitambo na magari yake ili kuongeza ufanisi.



Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA), Kanda ya Kati, Stella Rutaguza, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, katika semina kuhusu elimu ya aina za bima. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DC ataka walimu watesaji kukamatwa

**Na Mwandishi Wetu,**
MAKAMBAKO

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Ruth Msafiri, ameagiza kukamatwa kwa walimu watakaobainika kuwafanyia vitendo vya kikatili wanafunzi ikiwa hatua ya kukomesha vitendo hivyo vinavyoendelea nchini.

Msafiri alisema hayo jana mjini hapa wakati msafara wa kijinsia kutokomeza ukatili ulipofika mkoani Njombe kwa ajili ya kutoa elimu ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema serikali haipingi adhabu ya viboko lakini si kutoa adhabu hiyo kupitiliza na kusababisha ulemavu na maumivu kwa wanafunzi. Mkuu huyo wa wilaya alisema suala la ukatili wa kijinsia ni mapambano makubwa nchini, hivyo jitihada zinahitajika kwa wananchi, wadau na mashirika yasiyo ya kiserikali kuhakikisha wanaunganisha nguvu ili kuondokana na vitendo hivyo.

Alivitaka vyombo vya usalama kuacha kufanya ukatili kwa kuchelewesha kesi za vitendo vya unyanyasaji wa na kusababisha ukatili wa kihisia kwa waathirika wa matukio hayo.

"Vyombo vya usalama mnachelewesha kesi kwa sababu mnaomba rushwa. Nawaomba msiwe kikwazo cha kupatikana kwa haki ya wahanga (waathirika) wa vitendo vya ukatili," alisema. Akizungumza kuhusu msaada wa kisheria unaotolewa na Shirika la Legal Serivces Facility, Joseph Magazi alisema wameweka nguvu katika kuisidia jamii katika matatizo ya kisheria kwa kuwawezesha wasaidizi wa kisheria katika mikoa na wilaya kutoa elimu husika.

"Tumejipanga kushirikiana na serikali katika kuhakikisha tunaifikia jamii katika kutoa elimu itakayowezesha wenye matatizo mbalimbali ya kisheria kupata msaada na kuyatatua matatizo yao," alisema.



Mafundi wakiendelea kupaka rangi kwenye majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Ngorongoro, inayoendelea kujengwa mkoani Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wapata tiba kupunguza msongamano mahabusi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA MJINI

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Amon Mpanju, amezindua Jukwaa la Haki Jinai la Mkoa wa Arusha ili kuharakisha utoaji wa haki kwa watu mahakamani na mahabusu.

Akizungumza juzi katika hafla fupi ya uzinduzi wa jukwaa hilo, Mpanju alisema kufunguliwa kwake kutasaidia kupunguza mlundikano wa mahabusi gerezani.

"Mimi nawapongeza sababu hii ni moja ya hatua ya kushughulikia tatizo hili na mengine na watu watapata haki kwa wakati,"alisema.

Aliagiza wajumbe wa jukwaa hilo ambao ni viongozi wa vyombo vya ulinzi na usalama, kuongeza kasi ya kushughulikia wanaohujumu serikali kwa maslahi yao binafsi.

"Msiogope mtu yeyote mwenye cheo chochote, mradi hammwonei mtu, tekelezeni majukumu yenu na kuisaidia serikali na hapa Arusha nawapongeza maana mlishakamata watoroshaji wa madini ya Tanzanite waliokuwa wakipeleka Kenya," alisema.

Aliongeza kuwa Arusha ni kitovu cha utalii, madini mengi na mikutano ya kimataifa mingi, hivyo kuna kila sababu kuimarisha ulinzi ili kuwe na amani na usalama.

Kuhusu uchaguzi, Mpanju aliagiza kila mwananchi kufuata sheria na taratibu za nchi, ili kuimarisha usalama katika kuuendesha pamoja shughuli nyingine za kiuchumi.

Aliwataka wananchi kuwa makini katika kipindi cha uchaguzi mkuu mwaka huu kwa kutokujihusisha na makosa ya jinai.

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, alisema anaamini jukwaa hilo litasaidia kupambana na uhalifu mkoani hapa.

"Naamini huwezi kuwa na maendeleo bila kuwa na haki au kutenda haki kwa watu, hivyo kupitia jukwaa hili, watu watapata haki zao kwa haraka na kupunguza malalamiko ya mashauri kuchukua muda mrefu," alisema.

Aliagiza viongozi wa jukwaa hilo kuhakikisha wanahudhuria vikao viwili vya lazima kila mwaka bila kutuma wawakilishi ili kupanga mikakati ya kushughulikia uhalifu katika maeneo yao.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Franck Maisumbe, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alisifu kuzinduliwa kwa jukwaa hilo na kuahidi kutoa ushirikiano ili kazi zilizokusudiwa zifanikiwe.

Pia, aliipongeza Ofisi ya DPP kwa kuondoa urasimu na kuharakisha mashauri kwa lengo la kutoa haki kwa wakati kwa wananchi.

"Natarajia jukwaa hili litakuwa msaada kwa wilaya, mkoa na taifa katika kupunguza kero za wananchi katika mashauri yao, kwa sababu wananchi wanapochelewa kupata haki, wanaanza kuichukia serikali na kuilaumu,"

# Mtaalamu awapa neno wakulima msimu mpya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA MJINI

MRATIBU wa Uhamilishaji Teknolojia na Ushirikiano wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) na Kituo cha Seliani Arusha, Rose Ubwe, amewataka wakulima mkoani Arusha kushirikiana na maofisa kilimo, ili kupata ushauri jinsi ya kutumia mbegu zinazoendana na mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumzia msimu wa kilimo unaoanza mwezi ujao, mratibu huo, alisema jijini hapa juzi kuwa ni wakati mwafaka kwa wakulima kuandaa mashamba na kutumia mbegu bora zinazostahili ukame na mwelekeo wa hali ya hewa.

Alisema kituo hicho ambacho ni miongoni mwa vituo 17 vya Tari nchini, kimekuwa na mikakati ya usambazaji wa teknolojia kwa wakulima kupitia wataalamu wa kilimo kwenye kata na kushirikiana na wataalamu wa vijiji, ili kuwafikishia mbegu bora na mbolea.

"Ninachoomba ili mkulima afanikiwe, nawaomba wakulima wasikilize taarifa kutoka kwa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), ili kuendana na kilimo chenye tija na kuepukana na matatizo ya kupata hasara na kuvuna mazao machache baadaye," alisihi.

Alisema kilimo kinatajwa kuwa na mchango mkubwa nchini, hivyo Tari na Selian wanapenda kuona wakulima wanazitumia teknolojia zinazoshauriwa, ili kudhibiti wadudu wanaoshambulia mazao yao.

Pia, aliwahimiza wakulima kutumia dawa na kuwaona wataalamu pale inapobidi, ili kuisaidia nchi kuwa na chakula cha kuto-

# DED asifu utekelezaji wa ahadi za Rais JPM

**Na Mwandishi Wetu,**

**MBULU**

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Hudson Kamoga, amemshukuru Rais John Magufuli kwa kuwapatia fedha za miradi ya maendeleo, ukiwamo ya ujenzi wa hospitali ya wilaya na jengo la utawala la halmashauri.

Kamoga alitoa pongezi hizo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kwenye makao makuu mapya ya halmashauri ya wilaya hiyo yaliyoko Kata ya Dongobesh.

Alisema wanamshukuru Rais Magufuli kwa kuwapatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la makao makuu mapya ya halmashauri hiyo ambalo limefikia asilimia 70 ya ujenzi wake.

Alisema Rais Magufuli aliwapatia Sh. bilioni 4.7 za ujenzi wa jengo la utawala wa halmashauri hiyo, ambalo linajengwa na wanajeshi kupitia Kampuni ya Mzinga.

"Tunamshukuru Rais Magufuli kwani tulipopata fedha hizi, tulianza ujenzi Aprili mwaka jana na tunatarajia kukamilisha Aprili mwaka huu na kuanza kutumika," alisifu.

Alisema serikali pia iliwapatia Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya ambayo iko katika hatua za mwisho kulikamilika.

Alisema Kituo cha Afya Dongobesh pia kimeboreshwa baada ya kupatiwa Sh. milioni nne na kujengwa jengo la mama na mtoto ambalo ni maalum kwa kinamama kujifungua.

"Pamoja na hayo, tunamshukuru Rais Magufuli kwa kutimiza ahadi yake aliyoitoa wakati anagombea urais mwaka 2015 ya kuweka lami Dongobesh na Haydom," alisema.

Alibainisha kuwa kwenye Kata ya Dongobesh, tayari Km 600 za lami zimejengwa na mchakato wa kujenga Km 1.4 baada ya wiki moja ujenzi utaanza.



Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John Masunga (kushoto), akizungumza na maofisa na wakuu wa Zimamoto na Uokoaji, mkoani Manyara, akiwa katika ziara yake ya siku moja mjini Babati, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Marufuku kuzikana makaburi ya familia

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WAKAZI wa Mji Mdogo wa Hai mkoani Kilimanjaro, kuanzia sasa watalazimika kuzika ndugu na jamaa zao katika makaburi ya umma, baada ya serikali kukamilisha mchakato wa kutenga eneo maalumu la makaburi.

Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo, Noel Nnko, alisema jana kuwa katika eneo la ekari 10 ambalo litatengwa kwa shughuli mbalimbali, ameagizwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, kutenga walau ekari tatu ambazo zitatumika kwa ajili ya mazishi. "Kumekuwa na vilio vingi kwa muda mrefu. Nashukuru Mungu kwamba Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, juzi alitoa maelekezo baada ya maombi hayo kwamba kuna eneo la ekari 10 ambalo litatengwa. Sasa akanielekeza kwamba angalau ekari tatu au asilimia 30 ya eneo hilo ambalo tunalo, litengwe kwa ajili ya maziko," alisema.

Kwa mujibu wa Nnko, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Hai, amemwagiza kutekeleza agizo lake kabla ya Machi 15, mwaka huu. "Waheshimiwa Wenyeviti wa Vitongoji na Wajumbe wa Viti Maalum wa Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai, nawaahidi kwamba kwa maelekezo aliyonipa mkubwa wangu (Sintoo), naenda kufanyia kazi na tutapata eneo la maziko ambalo litakuwa la mamlaka kwa ajili ya kuwasitiri ndugu zetu watakaokuwa wamepoteza maisha," alisisitiza. Katika hatua nyingine, Nnko amesema ofisi yake imeanza mchakato wa kupita kila kaya kukabidhi miche 10 ya miti ambayo itapandwa kuzunguka makazi yao ili kuifanya Hai kuwa ya kijani. "Nitahakikisha hiyo miti 90,000 naileta kwa namna yoyote ili kuhakikisha mji wetu unakuwa kijani wakati wote. Kuna maeneo yameoteshwa miti utadhani si Boma unaweza ukajua ni uzunguni.

"Nimeleta miti 10,000 ioteshwe ionekane na ninyi wenyeviti mtaonekana mna thamani kubwa kama kutakuwa na miti kwenye maeneo yenu. Ukiotesha miti ng'ombe wanakula, sasa tukubaliane mtu mwenye mifugo aweke ndani, mjiongeze ili miti hiyo ionekane inaoteshwa," alisema.

Kampeni hiyo ya kuifanya Hai kuwa ya kijani, inalenga kubadilisha mtazamo watu na wapitaji wa barabara kuu ya Moshi-Arusha kudhani kwamba eneo hilo ni kame.

Zaidi ya watu 20,000 wanapita barabara hiyo kwa siku.

# Wataka kiwanda kuzalisha taulo za kike

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WADAU wa sekta ya afya wa Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wamewashauri wafanyabiashara wenye uwezo mkubwa kiuchumi kufikiria kuwekeza kiwanda cha kuzalisha taulo za kike katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

Kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wadau hao akiwamo Mchungaji Leonard Minja wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, walisema wakati serikali ikiwa imenuia kujenga viwanda vya kuzalisha taulo za kike kama hatua ya kumwezesha mwanamke kupata bidhaa hiyo muhimu, kuna kila sababu kwa wafanyabiashara wa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga kuchangamkia fursa hiyo.

"Si kila kitu tunapaswa kuiachia serikali. Nadhani hata hili la kiwanda cha kuzalisha taulo za kike linapaswa kuchukuliwa na wafanyabiashara ambao wana uwezo mkubwa kiuchumi. Tunashukuru wapo wenzetu wameanza kutoa misaada ya taulo hizo shuleni lakini ni vyema tukawa na viwanda vyetu," alisema Donacian Macha, mkazi wa Kibosho Road.

Mwishoni mwa mwaka jana, Wizara ya Fedha na Mipango ilisema serikali inakusudia kujenga viwanda hivyo mwaka huu mkoani Simiyu kwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Wakati wadau hao wakitoa pendekezo hilo, pia juzi Taasisi ya Maendeleo ya Uru (UDF), ilitangaza kuanzisha kampeni maalum ya kimkakati ya 'Binti Nabaki Darasani.'

Kampeni hiyo imepewa jukumu la kutafuta fedha za ununuzi wa taulo za kike kwa ajili ya kuwafikia zaidi ya wanafunzi 4,000 wanaosoma shule za sekondari katika Wilaya ya Moshi.

Akizungumzia kampeni hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Wakili Wilhard Kitali, alisema katika awamu ya kwanza ya kampeni hiyo itakayozinduliwa Machi 9, mwaka huu, wanafunzi 500 kutoka shule za sekondari za Mangi Sabasi, Mawella na Chuo cha Ufundi Mawela (MVTC) watanufaika na taulo hizo au kwa jina jingine sodo.

Alisema katika mgawo wa taulo hizo za kike, wanafunzi wa shule tatu ambazo ni Mangi Sabasi watapata taulo 200, Mawela 250 na Chuo cha Ufundi Mawella watapewa taulo 50.

# Wakulima kusajiliwa kidijitali

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WAKULIMA wa mazao ya chakula na biashara katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, wataanza kusajiliwa mwaka huu kwa njia ya mfumo wa kielekroniki kupitia mpango wa 'Yetu Wote' unaolenga kumsaidia kutambua jasho lake na masoko.

Ofisa Tawala wa Wilaya ya Hai, Mary Mnyawi, aliyasema hayo jana wilayani hapa, alipokuwa akizungumza na wataalamu wa kilimo kuhusu adhima ya serikali kukuza sekta hiyo.

"Lengo la mpango huu ni kufanikisha kazi ya kuimarisha ubora wa mazao, kutafuta masoko na kuimarisha bei ya mazao na hatimaye kuboresha uchumi wa wakulima na jamii iliyopo kwenye mnyororo wa mazao husika.

"Serikali tayari imegharamia mafunzo maalumu kwa wataalamu na mmeelekezwa namna ya kutumia mfumo wa kielektroniki ambao unafuatilia kwa karibu shughuli zote za shamba. Kimsingi mpango huu unafanya kazi ya kumsajili mkulima na mashamba yake chini ya kundi (Amcos) la zao husika," alisema.

Aidha, Mnyawi aliwataka wataalamu hao wa kilimo kuwa na mipango endelevu ya utoaji elimu kwa wananchi wanaojishughulisha na shughuli za kilimo na mifugo.

Alisisitiza kuwa utaratibu huo utawasukuma wakulima na wafugaji kuzalisha kwa kiwango bora kitakachowasaidia kuingia katika ushindani wa soko la mazao na mifugo katika masoko ya nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Elia Machange, aliwataka watumishi wa idara za kilimo na mifugo kutumia ujuzi walioupata kwenye mafunzo hayo, huku pia akiwakumbusha watumishi kuendelea kutimiza wajibu wao kwa wananchi na kuwapa huduma kulingana na mahitaji.

Wakati serikali ikija na mpango huo wa usajili wa wakulima, kwa upande wao wataalamu wa kilimo na hasa maofisa ughani wako katika wakati mgumu kufikia malengo ya Wizara ya Kilimo ya kuongeza mchango wake kwenye uchumi wa viwanda kutokana na kukosa vitendea kazi.



## TIRA yataka kujiepusha udanganyifu

Na Augusta Njoji, DODOMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), imewataka Watanzania kujiepusha na udanganyifu watakapokata bima za mali zao kwa kuwa inasababisha kukosa fidia stahiki.

Rai hiyo ilitolewa jana na Meneja wa TIRA Kanda ya Kati, Stella Rutaguza, katika warsha ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuhusu kuandika habari za bima ili kusaidia wananchi kupata uelewa.

Alisema udanganyifu huo unasababisha kulipwa fidia kidogo chini ya hasara wanayopata.

Aidha, alisema kumekuwepo na utata wa thamani ya vyombo ikiwamo ndege za kisasa na kusababisha ugumu kwenye utendaji kazi wao.

"Mtu anaweza kudanganya chombo hiki kina thamani hii, inalazimu kutumia wataalam kujua thamani halisi ili kujiepusha na gharama za udanganyifu,"alisema.

Alisema katika ndege za kisasa, imekuwa ni vigumu kujua gharama halisi ya chombo husika hali inayopelekea kutumia wataalam wa anga.

Sambamba na hilo, meneja huyo aliwataka Watanzania kujiunga na bima mbalimbali ili kupunguza makali ya hasara yanayotokana na majanga.

Alisema waandishi wa habari wanawajibu wa kutoa elimu kuhusu umuhimu wa bima na faida zake ili wananchi wajiunge ikiwemo ya mikopo, elimu, magari, mazishi na mitaji kwa kuwa kila kitu kinahitaji bima.

Alifafanua kuwa kuna bima ya mazishi, ingawa Watanzania wanaogopa lakini ni nzuri inasaidia kubeba gharama za mazishi badala ya kukimbizana na michango.

"Elimu ya bima kwa wanahabari ni kiungo muhimu kwa mamlaka ya usimamizi wa bima na wananchi wanaopewa huduma, mkiwa na uelewa mtatusaidia kufikisha uelewa kwa wananchi, sisi tukaona ni muhimu kupata elimu hii ili kuwasaidia wananchi kwenye majukumu yetu,"alisema.

# Wamiliki viwanja hatarini kupokwa

Na Augusta Njoji, CHEMBA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chemba imetoa siku saba kwa zaidi ya wamiliki 400 wa viwanja na taasisi 14 kulipia gharama za viwanja hivyo kabla ya kuchukuliwa hatua za kisheria.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Semastus Mashimba, alipokuwa akizungumzia taasisi na wamiliki hao walioshindwa kulipa kulingana na muda uliopangwa.

Dk. Mashimba aliwataka wale wote waliohodhi viwanja ambavyo havijalipiwa, kulipa kabla ya hatua za kisheria kuchukuliwa.

"Bila kufanya hivyo, viwanja vitachukuliwa na kugawiwa kwa watu wengine na taasisi zingine. Watu hao wahakikishe wanatumia muda huo wa siku saba kuanzia leo (jana) kulipia kabla ya kuporwa," alisema.

Ofisa Ardhi na Maliasili wa Halmashauri hiyo, Enock Mligo, alisema sheria ya ardhi imetoa miongozo na taratibu lazima kulipia kiwanja.

"Yeyote anayemiliki kiwanja ndani ya halmashauri, jiji, manispaa au mji anapaswa kulipia kwa mujibu wa sheria," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema awali ulitolewa muda wa siku 30 kwa watu waliochukua viwanja kwenye wilaya hiyo kulipia lakini wako ambao hawajalipia.

"Kutokana na hili sasa Baraza la Madiwani Chemba likatoa siku saba kwa wananchi wote wanaodaiwa viwanja kulipa ndani ya muda huo,"alisema.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, akizungumza katika Kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma juzi, alipofika wilayani humo kwa ziara ya kikazi. **PICHA: WMNN**

# Shule 10 Dodoma zapewa vishkwambi 700

Na Augusta Njoji, DODOMA

SHULE 10 za msingi za serikali na binafsi jijini Dodoma, zimepatiwa vishkwambi 700 ili kuongeza chachu ya wanafunzi kufanya vizuri kwenye masomo yao.

Vishkwambi hivyo vimetolewa na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu akishirikiana, Taasisi ya Don Bosco na Shirika la Profuturo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa ugawaji wa vishkwambi kwa wanafunzi ili kujifunza kusoma kielektroniki.

Akizungumza jana katika hafla ya ugawaji vifaa hivyo, akimwakilisha Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alisema hatua hiyo itasaidia kupaisha sekta ya elimu katika wilaya hiyo.

Katambi alizitaka shule zilizonufaika na msaada huo kuvitunza vifaa hivyo na kuvitumia kuchochea ufaulu kwa wanafunzi.

"Lazima Dodoma iwe tofauti na majiji mengine kiteknolojia na katika hili Mavunde umefanya kwa vitendo, nakupongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kutatua matatizo ya elimu na kuwakomboa wananchi wako kielimu," alisema.

Kwa upande wake, Mavunde alishukuru Profuturo kwa kuchangia sekta ya elimu na mkakati wa kulifanya jiji la Dodoma kama moja ya maeneo ya matumizi ya sayansi na teknolojia.

Alisema kutolewa kwa vishkwambi katika shule ni awamu ya pili ya muendelezo wa kuimarisha ufundishaji kwa kutumia mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) ambapo awali vilitolewa 5,000 kwa shule 10.

Alibainisha ndoto yake kila siku ni kuona Jiji la Dodoma linapiga hatua kubwa kwenye elimu kwa kuzalisha vijana wengi wanaofaulu vizuri kwani anaamini kupata kwao elimu bora ndio njia ya wao kufanikiwa kwenye maisha na kuwa msaada kwa taifa.

Mavunde alisema ataendelea kutoa vifaa hivyo kwa shule zingine katika awamu zijazo ili watoto wa Dodoma wapate uelewa wa matumizi ya teknolojia wakiwa bado wadogo.

Akitoa maelezo ya mradi, Mwakilishi wa Don Bosco Net, Padri Peter Mutechura, alisema vishkwambi hivyo vinagharimu Sh. milioni 700 na vinalenga kuwanufaisha wanafunzi hao kuwa na uwezo wa kutumia teknolojia wakiwa katika umri mdogo.

"Tunaahidi kuendelea kushirikiana na Mbunge Mavunde kutatua changamoto za elimu jimbo la Dodoma mjini,"alisema.





Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, akiahirisha Mkutano wa Kumi na Saba wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Zanzibar, katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani Nje kidogo ya Mji wa Zanzibar juzi, uliojadili Miswada pamoja na Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza hilo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Samia aonya wasiostahili kuandikishwa kupiga kura

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amesema kazi ya uandikishaji wapigakura wapya na uhakiki wa taarifa za wapigakura waliomo katika daftari la kudumu ni lazima ihakikishe na raia wa Tanzania ndio wanaopiga kura na si raia kutoka nchi zingine.

Akizungumza baada ya kufanya uhakiki wa taarifa za wapigakura katika daftari la kudumu katika kituo cha Shule ya SOS Wilaya ya Magharib 'B' Unguja, alisema kila nchi lazima ijue raia wake kupitia vitambulisho.

Samia aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la wapigakura ili wasipoteze haki zao za msingi.

"Bila ya kujiandikisha katika daftari na kuhakiki taarifa zako, utakosa haki ya demokrasia ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu ujao wa mwaka huu," alisema.

Samia alipongeza utaratibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika vituo vya kuhakiki taarifa hizo kutokana na kutokuwapo usumbufu wa aina yoyote na kila mwenye sifa anapata haki yake.

"Sukutegemea kabisa kama kazi hii itatachukua muda mfupi tu. Nilijua nitatumia zaidi ya robo saa lakini hata dakika tano hazijafika nimeshamaliza kuhakikiwa taarifa zangu," alisema.

Baadhi ya wananchi wa shehia ya Mombasa waliofika kituoni hapo kuhakiki na kujiandikisha katika daftari hilo, walisema kuwa kazi hiyo inaendelea vizuri.

Kuhusu wananchi waliokosa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, Mkurugenzi Uchaguzi kutoka Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Thabit Idarus Faina, alisema tume itabandika orodha ya majina katika ofisi za wilaya au eneo lolote ambalo itaelekeza ili kupewa fursa ya kurudishwa katika daftari na kupata haki zao za msingi.

# SMZ yajivunia mafanikio kupitia Tasaf

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, amesema mafanikio makubwa yamepatikana kupitia utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (Tasaf).

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana, alisema jamii imekuwa shahidi kutokana na mafanikio hayo yaliyopatikana ndani ya mpango huo.

Alisema ni vyema wananchi waendelee kushirikiana na viongozi katika kuyatunza mafanikio hayo hatua kwa hatua yanayotokana na mradi huo uliojitokeza bayana kuwa ni mkombozi wa wananchi wanyonge.

Balozi Iddi aliwataka wananchi kuendelea kujenga uaminifu, ukweli na uadilifu katika hatua zote za mradi kuanzia ukusanyaji wa taarifa za walengwa watakaotimiza vigezo ili wapate fursa hiyo katika ngazi zao.

"Nina furaha kueleza kwamba awamu ya pili ya mpango wa kunusuru kaya maskini (Tasaf III – II) inayotegemewa kutekelezwa kwa miaka minne tayari ilishazinduliwa rasmi na Rais Dk. John Magufuli hivi karibuni.

Makamu huyo wa Pili wa Rais alitoa wito kwa watumishi wote watakaoshiriki katika ngazi tofauti za mradi huo waonyeshe uzalendo wao na serikali haitamfumbia macho mtumishi atakayebainika ameshiriki kwa njia yoyote katika kuchangia upotevu au ubadhirifu wa fedha za mradi huo. Kuhusu utabiri wa kuwepo kwa mvua kubwa zinazotarajiwa kunyesha wiki ya pili ya mwezi ujao ya msimu wa masika uliotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Balozi Iddi aliwataka wananchi kuendelea kukumbushana umuhimu wa kuzitumia vizuri mvua hizo.

Alisema licha ya taifa kuendelea kupata mvua katika kipindi hicho kwa baadhi ya wakati, bado jamii hasa wakulima ni vyema wakazitumia mvua hizo kwa shughuli za maendeleo zikiwamo kilimo cha mazao ya chakula na miti ya kudumu.

Aidha, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari za kujiepusha na maafa kwa kuhama mapema kwenye maeneo hatarishi, kufuatilia mienendo ya watoto wao, kufuata maelekezo ya wataalamu wa Mazingira, afya na kuendelea kufuatilia taarifa za kitaalamu na elimu zinazotolewa na TMA.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walipokea, kuchangia na hatimaye kupitisha miswada miwili ya sheria, ripoti tisa za kamati za Baraza hilo, Taarifa ya Dawa za Kulevya na marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Baraza hilo la Wawakilishi lililopokea Maswali 112 ya Wajumbe wa Baraza hilo na kujibiwa. Baraza hilo limeahirishwa hadi Aprili Mosi, mwaka huu.

# Mafunzo utalii yaongeza tija

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

PROGRAMU ya mafunzo ya uanagenzi kwa vijana wanaotaka ajira katika sekta ya utalii visiwani Zanzibar, imeelezewa kuwa imepata mafanikio makubwa.

Mratibu wa Mafunzo Kazi kwa ajili ya Hoteli Zanzibar, Adil George, alisema programu hiyo inayolenga kumaliza kilio cha ukosefu wa ajira za hoteli kwa vijana wa Zanzibar, imepunguza malalamiko kwa kiasi kikubwa.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo kwa wasimamizi wa hoteli mbalimbali zitakazopokea wanafunzi wa awamu ya pili ya programu hiyo yanayofanyika hoteli ya Double Tree mjini Zanzibar, George alisema vijana 170 wamepatiwa mafunzo tangu kuanza kwa programu hiyo Agosti, 2017. Alisema miongoni mwa vijana hao, zaidi ya asilimia 60 wamepata ajira katika hoteli mbalimbali za kitalii, zikiwemo zile ambazo baadhi ya wahitimu walipitia kwa mafunzo ya vitendo.

Mratibu huyo alilishukuru Shirika la Kazi Duniani (ILO) linaloendesha programu hiyo kwa ufadhili wa serikali ya Norway kwa kukubali mafunzo hayo yawe endelevu ikiyasimamia kwa awamu ya pili sasa.

Aidha, alieleza kufurahishwa na hatua ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, kwa kutoa ushirikiano wa kila hali kuhakikisha programu hiyo inaendelea kwa ufanisi unaotarajiwa.

Mradi huo uliingia awamu ya pili iliyoanza mwaka 2019 na wanafunzi wanaendelea na mafunzo katika Kitivo cha Utalii cha Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), umejikita kutoa taaluma kwa nadharia na vitendo kwa vijana wanaokidhi vigezo ili wanapohitimu waweze kukubalika katika ajira za hoteli au kujiajiri wenyewe.

Akizungumza na wasimamizi wa idara mbalimbali za hoteli wanaopewa mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii Zanzibar (ZATI) inayoratibu programu hiyo, Helen Peek, alisema ili kupata wahitimu wazuri, ni lazima watendaji wa hoteli waelewe mbinu za kuwasaidia.

"Lazima mwalimu afunzwe njia na maarifa ya kukabiliana na wanafunzi, kwani kufanikiwa kwao ni sifa kwa hoteli wanazofanyia kazi, lakini pia kutaongeza vijana wenye sifa za kuajiriwa hotelini au kujiajiri," alisema.

Aidha, alisema hatua ya kudhamini mafunzo kwa vijana wa Zanzibar, inalenga kuhakikisha wanatanua elimu na kupata ujuzi utakaowezesha kuchukua nafasi za ajira za kitalii ambazo zimekuwa zikidaiwa kuhodhiwa na wageni wengi zaidi kuliko Wazanzibari.



**CARDI B ATANGAZA KUTUMBUIZA TENA AFRIKA**

Soma UK.20

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI FEBRUARI 29, 2020



## WEMA! WEMA!

# Shaka tele kama kakonda au kawa 'kipotabo'

BASI SAWA

# Mo Music hizo kiki bhana!

MWANAMUZIKI wa kizazi kipya, Mo Music, amesema anapenda kuringa na anajisikia raha.

Akizungumza na EATV, Mo Music amesema huwa anapata furaha pale mashabiki wanapomuuliza kwanini harudi kwenye muziki.

"Tayari nimeshaacha alama na sijawahi kushuka kimuziki, mpaka Dunia inapinduka hakutakuwa na Mo Music mwingine, halafu mimi napenda kuringa na hakuna kitu kizuri kama shabiki anakuuliza kwanini haurudi, kwa hiyo wanakuwa wanakumiss na una nafasi yako" ameeleza Mo Music.



# Stara akerwa matusi Bongo Fleva

MWANAMUZIKI mkongwe, Stara Thomas, amesema muziki wa Bongo Fleva umepoteza mwelekeo kutokana na wasanii wengi kuimba nyimbo zinazokiuka maadili.

Akizungumza na BT, Stara amesema licha ya muziki huo kupiga hatua, lakini kuna umuhimu kuangalia upya maudhui na maneno mazuri ili kuwalinda watoto.

"Wasanii wengi wa sasa wanaimba matusi, hii haipendezi kwani hata watoto wanaosikiliza nyimbo wanayoimba na kuleta hofu kwa kizazi kijacho. Turudi katika maadili kwa ajili ya ustawi wetu," amesema Stara.





# Mabantu kwani kweli mnajichubua?

WANAMUZIKI wanaounda Kundi la Mabantu. Muuh na Twaah, wametoa mpya baada ya kudai rangi waliyonayo katika miili yao wamerithi kutoka kwa wazazi.

Wasanii hao wamesema weupe wao hautokani na kujichubua na huwa wanakerwa na baadhi ya watu wanaotumia mitandao kuwachafua.


"Sio kweli, sisi hatufanyi hiko kitu, wanasema tunajichubua na unavyoniona mimi hata baba yangu yupo hivihivi, ni rangi za ukoo tu na mafuta ninayotumia, nywele ninaweka mafuta ya nazi tu situmii losheni wala nini" Muuh Mabantu.

## INSTA-TWITTER





**Fukara** ninayeshukuru, Tajiri nisiyekufuru, najua Hustle najua Bata, Mi' ni njiwa na kunguru- **Ben Pol.**



**Mhhh dhahama,** ng'ombe kagoma kuliwa, anasema na mchinjaji- **Baba Haji.**

UNASEMAAA...

# Idris eti ni kweli IST sawa na tiketi ya Superbowl?

MSANII wa vichekesho, Idris Sultan, amewaambia Watanzania kwamba kama mtu anataka kwenda kutazama mchezo wa Superbowl nchini Marekani, basi itamlazimu kulipa fedha sawa na ile ya kununua gari aina ya IST kukata tiketimoja.

Idris Sultan amesema hayo kwenye uzinduzi wa filamu yake mpya, wakati akielezea uzoefu alioupata alipoenda kutazama mchezo huo jijini Miami, Marekani siku kadhaa zilizopita.

"Sijawahi kujiona mnyonge maishani kama nilivyokuwa kwenye Superbowl, kwanza ni mchezo ambao unawatazamaji milioni 96 kwa wakati mmoja, tiketi yangu ya kwanza ilikuwa ni dola 5,000 sawa na Tsh Milioni 11 bahati mbaya nikapoteza, nikaja kuchukua nyingine ya dola 3,000" amesema Idris Sultan.

Akaongeza kwamba "Nikawa najiuliza mwenyewe uwanja umejaa zaidi ya watu 69,000, tiketi ya chini kabisa ni dola 2500 sawa na Sh. milioni 6, hiyo unanunua IST".





## Nay wa Mitego Mungu anakuona

RAPA mwenye utata mwingi, Nay Wa Mitego, amesema uongozi wa msanii wa Singeli, Meja Kunta, wanatakiwa kuchunguzwa kiakili kutokana na kitendo chao cha kutangaza kifo cha mwanamuziki wao kama njia ya kutafuta kiki.

Amesema kitendo cha kujizushia kifo ni bora angefariki kiukweli ili watu wangejua moja na kuendelea na mambo mengine kuliko vile alivyofanya yeye na uongozi wake.

"Niliangalia kiasi gani ile taarifa ilivyotoka na watu walivyoumia kuhusu yeye, watu walipata mshtuko, bado alikuwa msanii mchanga, pia mimi ni mmoja wa watu ambao nilisafiri naye kwenye siku hiyo ya tukio lenyewe ambapo ndipo walidanganya kama wamepata ajali na nilikuwa najua kinachoendelea" ameeleza Nay Wa Mitego

"Hata mimi nilipomsikia meneja wake amesema ni kweli amefariki nilipata mshtuko, ila baadaye nilipopata taarifa za chinichini kwamba ni mchezo wanatuchezea nikasema bora huko alipo afariki kiukweli kabisa, hata wale watu aliokuwa naye bora wangemzimisha," ameongeza.

## INSTA-TWITTER



**Dada** zangu niwaambieni kitu? Siyo kisa umedate naye muda mrefu ndiyo udhani atakuoa. Mimi nina mjomba wangu kasomea medicine miaka sita. Ila sasa hivi ni DJ-**Roma Mkatoliki.**




**Haijalishi** una mri gani, ukishaanza uhusiano, inabidi ukajitegemee-**Mboto.**



**Tafakari t**abia nchi, jua linawaka, sembe imepanda, wali utausikia kwenye radio-**Kingwendu.**

Kuumbe!

# WEMA! WEMA!

# Shaka tele kama kakonda au kawa 'kipotabo'



WASIWASI umetanda kwa mashabiki wa mwigizaji nyota wa Bongo Muvi, Wema Sepetu, kutokana na mwili wake kupungua kwa kasi kila kukicha.

Kutokana na hali hiyo, mitandao ya kijamii imekuwa 'bize' watu wakijadili suala hilo huku baadhi ya mashabiki wake wakihoji dawa anazotomia mrembo huyo na kumsababishia kupungua kiasi hicho.

Hata hivyo, mrembo huyo ameibuka kuondoa wasiwasi huo, akisema yupo buheri wa afya na kupungua kwake haijatokana na ugonjwa.

Kuibuka kwa Wema kutolea ufafanuzi suala hilo, inatokana na watu wanaomfuatilia kutilia shaka kupotea kwa uzito wake kwa kasi ya ajabu na kumfanya aonekane kama binti mdogo. Wema amesema aliamua kupunguza uzito wa mwili wake kutoka kilo 109 hadi kufikia 65 ambazo anazo kwa hivi sasa.

Kulingana na msaanii huyo kwamba yuko fiti na anafurahia mwili wake huo, kuliko alivyokuwa huko nyuma.

"Mimi nipo fiti sana, siumwi kitu na sina ugonjwa wa aina yoyote, mwili wangu mnaouona sasa naupenda kuliko miili yote ambayo mmewahi kuniona nayo, watu walianza kunijua kama Miss Tanzania nikiwa na mwili huu," amefafanua.

"Halafu nikanenepa wakanizoea vile japo kulikuwa na comments tofauti lakini naamini ni mazoea tu" ameongeza kusema Wema Sepetu.

Amewataka watu kuvuta subira kwani itafikia wakati watamzoea akiwa na mwili huo na kuona jambo la kawaida.

"Hata huu mwili naamini itafika muda watu watanizoea tu, kwamba nimekuwa kipotabo, nilikuwa nataka nirudi kwenye umbo lile la urembo," amesema.

Kulingana na maoni yanayotolewa katika mitandao ya kijamii, baadhi ya watu wanahoji kwa nini msanii huyo anazidi kupungua mwili na kupoteza lengo lake halisi la kuondokana na unene. Baadhi walimshauri kuonana na wataalamu afya ili kujiridhisha yupo salama, na endapo atapatikana na matatizo basi tafute tiba ya haraka kujinusuru.

# Wanaotoka na kiki kabla ngoma



BEN POL



MAKABILA



MAUA

**Na Adam Fungamwango**

MIAKA ya hivi karibuni kumezuka na tabia ya baadhi ya wasanii wa bongo fleva kufanya kwanza kiki kabla ya kuachia ngoma.

Maana ya kiki ni mtu kufanya jambo lolote lile ambalo si la kawaida, au tukio ambalo litawafanya mashabiki wake wasisimke.

Wasanii wengine wanafanya mambo makubwa ambayo kwao yanawadhalilisha, lakini hawajali, mradi tu wana lengo lao.

Lengo ni wakati watu wako kwenye mjadala, anatoa ngoma ambayo itakimbiliwa na kutazamwa na hadhira hiyo hiyo ambayo iko kwenye mjadala.

Nia ni kwamba ngoma hiyo iweze kutazamwa na kushabikiwa na wengi kwenye mitandao, redioni na TV, bila kuangalia ufundi wa vyombo, uimbaji na maudhui.

Nasikia siku hizi hata wanamuziki wakubwa duniani wanafanya hivyo. Hapa Tanzania wapo wasanii ambao wamefanya vituko vinavyoonyesha kuwa walikuwa na lengo la kuvuta hadhira ya mashabiki ili ngoma zao watakazotoa 'zihiti'. Hawa ni baadhi ya wasanii na ngoma zao waliozitoa.

**BEN POL-TATU**

Ilikuwa mwaka 2017 mwezi Mei kwenye mitandao ya kijamii ilipoanza kuvuja picha ya msanii Ben Pol akiwa nusu utupu.

Picha hiyo ilisambaa kwa kasi kama nzige wale wa Kenya. Ni picha ambayo ilionekana kama amejifunga minyororo, lakini akiwa nusu utupu.

Kila mtu aliongea lake. Lakini wenye kuangalia mambo haya kwa jicho la tatu, walijua kabisa kuna kitu. Mwezi mmoja baadaye akatoa ngoma yake mpya, na picha za video zikionyesha baadhi ya taswira iliyoonekana kwenye zile picha. Ngoma akaiita 'Tatu'.

**MAUA SAMA-IOKOTE**

Kiukweli kabisa msanii huyu hakuwa na nia ya kiki kwenye ngoma yake hii. Nia ilikuwa ni kama promo tu. Akatoa kipande cha video cha ngoma yake ya Iokote ambayo tayari alikuwa ametoa audio yake mwezi Septemba 2018.

Kipande hicho kilipotoka, alikamatwa na Jeshi la Polisi kwa kosa la uharibifu wa mali ya umma, kwa madai ya kuonekana kwenye mitandao ya kijamii wakizirusha pesa za Kitanzania na kuzikanyaga.

Maua Sama na waliohusika walisota mahabusu kwa siku kadhaa, lakini wakaachiwa.

Hiyo pekee kwao bila kutarajia ilikuwa kama kiki ya aina yake. Kwani mwezi uliofuata, Oktoba mwanzoni tu, video ya ngoma ya Iokote ikatoka na kuwa gumzo nchini.

**MEJA KUNTA-WANGA**

Mwaka huu huu, mwanzoni mwa Februari zilizuka habari za kifo cha msanii, mwimbaji wa muziki wa singeli.

Tena waliotoa habari hizo za kifo ni mmoja wa mameneja wake ambazo alizitoa kwenye mtandao wake wa kijamii. Zilisambaa hadi kwenye redio na televisheni, kiasi baadhi ya mashabiki wake walianza kulia na wengine kutuma salamu za rambirambi. Ukweli ni kwamba Meja Kunta alipata ajali, lakini hakufa.

Kwa nini azushiwe kifo? Februari 13 akatoa ngoma mpya aliyoiita 'Wanga'.

**DULLA MAKABILA-NINGEKUWA DEMU**

Wiki mbili tu zilizopita, msanii wa ngoma za Singeli, Dulla Makabila alitoa ngoma iitwayo 'Ningekuwa Demu'. Hii ni baada ya sintofahamu ya wiki mbili nyuma ya picha zilizovuja mitandaoni zikimuonyesha akiwa amejipodoa kama mrembo fulani hivi.

Ubishi ulikuwa mkubwa kwenye mitandao kuwa huyu ni Dulla na kujiuliza ni kwa nini amefanya vile, wengine wakibisha kutokana na jinsi alivyopambwa na kurembwa na kudai si mwenyewe, mwenyewe akiwa kimya kabisa, kabla ya ngoma hiyo kutoka. Kumbe ilikuwa ni kiki.

## IMETOKEA

# Duh! Mwanamke aolewa na wanaume wawili, kila mmoja azaa naye watoto

MVUTANO mkali wa kimapenzi umeibuka katika jimbo la Kano nchini Nigeria, baada ya wanaume wawili kujikuta wameoa mwanamke mmoja kwa nyakati tofauti.

Mwanamke huyo, Hauwa Ali Mariri, mwenye umri wa miaka 32, sasa anahofia kupata adhabu iwapo atapatikana na hatia ya kuwadanganya wanaume hao.

Kano ni mojawapo ya majimbo kadhaa ya Nigeria ambayo yanaongozwa kupitia sheria ya Kiislamu na ni makosa kwa mwanamke kuolewa zaidi ya mwanamume mmoja.

Kufichuka kwa siri hiyo kunatokana na Bello Ibrahim (40) mume wa kwanza wa Mariri aliporudi nyumbani na kumpata mwanamume mwengine amelala katika kitanda chake.

Ibrahim alikuwa ameugua kwa muda mrefu na alikua ameondoka kijijini hapo kwa ajili ya kupata matibabu ambapo huko alikaa kwa muda wa miaka miwili.

Anamtuhumu Mariri kwa kufunga ndoa bila yeye kujua. Aliiambia BBC kwamba walitalakiana.

"Alisema kwamba ameniwacha kabla kuondoka kijijini. Ndio maana nilifunga ndoa na Bala, nilihisi kwamba nilikuwa huru aliposema kwamba amenipa talaka", alisema.

Hatahivyo, Ibrahim amekana akisema kwamba hakumpa talaka na anamtambua bado ni mkewe.

Wawili hao walifunga ndoa miaka 17 iliyopita na walifanikiwa kupata watoto sita.

Ibrahim amesema hakuna ushahidi kwamba alimuacha mkewe na kuhoji talaka aliyompa iko wapi?

"Sikumuwacha. Iwapo anasisitiza kwamba nilimpa talaka ushahidi uko wapi, barua niliomuandikia iko wapi?",

Talaka nyingi nchini Nigeria hutolewa kwa mdomo ama kupitia barua.

Ibrahim ambaye amesema amevunjika moyo aliwasilisha malalamiko yake polisi wa jimbo hilo ambao wamekiri wanachunguza tukio hilo.

Kwa upande wa mumume wa pili, Bala Abdulsalam (35)0, alisema mkewe Mariri alimwambia alikuwa ameachana na mumewe na kwamba yupo tayari kufunga ndoa.

Amesema alimtumia dola za Marekani 50 kusimamia ndoa hiyo pamoja na mahari.

"Nilikuwa nje ya mji wakati nilipomtumia fedha hizo, niliporudi Kano alikuwa mke wangu", aliambia BBC.


Pamoja na hayo, amekuwa na wasiwasi kuadhibiwa iwapo mahakama za sheria zitampata na hatia kwa kumuo mke wa mtu.

Uhusiano huo wa miaka miwili ulisababisha kuzaliwa kwa mtoto mmoja na wakati huu Mariri ni mjamzito na mtoto wa pili.

Mwanamke huyo ameondoka katika nyumba aliyojenga na mume wake wa kwanza na kuwaacha watoto sita na mumewe, huku mume wa pili akitakiwa na polisi kutoondoka Kano mpaka uchunguzi ukamilike.

Gwani Murtala , Kamanda wa Kituo cha Polisi cha Kumbotso, amesema kesi hiyo ni ya kwanza kuwahi kufanyika na kwamba hajui jinsi itakavyomalizwa.






## DNA

# Walimwengu wana mengi

**Na Adam Fungamwango**

WENGINE wanasema dunia hadaa. Wapo wanaosema, dunia tambara bovu. Baadhi wanasema dunia hadaa ulimwengu shujaa. Kuna wanaosema dunia uwanja wa fujo, mwenye ngoma zake acheze zipasuke.

Wote hao maana yao ni moja. Ni kwamba duniani kuna mambo mengi ambayo wakati mwingine hayana uhalisia wa wewe unavyoyaona. Mkweli anaweza kugeuzwa kuwa muongo na jamii ikaamini na hata kumuua. Muongo anaweza kugeuka kuwa mkweli na kuaminiwa na jamii, kiasi kuwafanya wakweli wote kuonekana hawana maana.

Ni kweli kuna msemo unasema ukweli hata kama ukichelewa, lakini utafika tu, lakini wakati mwingine unafika wakati ambapo mkweli tayari ameshahukumiwa kwa uliokuwa unadaiwa uongo. Wakati mwingine anakuwa ameuawa kabisa, hivyo hawezi kurudi.

Ndani ya filamu ya DNA kuna mkasa mzito wa JB na mkewe Cathy. Ndani ya filamu hiyo pia kuna Selemani Barafu, Riyama Ally na mwanamuziki Banana Zorro.

JB na mkewe Cathy wanaishi maisha ya raha na amani. Hata hivyo siku moja Cathy anakutana na Barafu, mwanamume ambaye walishawahi kuwa kwenye semina moja, kabla hajaolewa.

Wote wanakumbukana na kufurahi. Barafu anavutiwa na Cathy na kumuuliza kama ameolewa.

Baada ya kusikia tayari ameolewa, Barafu anajisikia vibaya, pia anapomtaka Cathy kuvunja amri wa sita, anakataa kwa madai hawezi kuisaliti ndoa yake.

Hilo linamnyima sana raha Barafu mtu mwenye pesa zake na utajiri, na kuamua kumkomoa. Lengo ni kutaka kuiharibu kabisa ndoa hiyo.

Kinachofanyika ni kwamba, inaandikwa barua ya uongo kwenda kwa Cathy ili kuonyesha kuwa mtoto huyo ni wa Barafu na si wa JB, hivyo mwenyewe anamhitaji mtoto wake.

Barua hiyo inamfikia JB, naye kama binadamu sasa akataka ajidhihirishe kama yule mtoto wa kike aliyezaa na Cathy ni wa kwake kweli. Akaamua kumchukua mkewe na mtoto kwenda hospitali kwa ajili kufanya vipimo vya DNA.

Barafu aliyepanga mpango huo, anatuma tena watu kumteka mtoto wa daktari mkuu ambaye ni Banana.

Aliporejea nyumbani hamkuti mtoto, badala yake anakuta barua ikimtaka kubadilisha matokeo ya vipimo vya DNA, badala ya kuandika mtoto ni wa JB, aandike si wa kwake, ili aamini kuwa ni wa Barafu. Lengo ndoa ivunjike na Barafu achukue mzigo.

Hata hivyo, mpango unaingia dosari baada ya watekaji kukamatwa wakiwa na mtoto wa daktari.

Walikamatwa wanamtaja aliyewatuma, ambaye ni Barafu, ndipo mpango mzima wote unafichuliwa na wahusika wote, wakiwa chini ya uongozi wa Selemani Barafu wanatiwa mbaroni.

Hiyo ikawa nusura ya ndoa ya JB na mkewe Cathy ambayo tayari ilikuwa imeshafitinishwa.

Daktari akamchukua mtoto wake na kurejea naye nyumbani, JB, mkewe na mtoto wao nao wakarejea kwenye furaha yao ya awali.



USHETANI WA WEINSTEIN

# Alilazimisha ngono, sasa asubiri kifungo

MTAYARISHAJI maarufu wa filamu kutoka Hollywood, Harvey Weinstein, anaweza kukaa kwa miaka mitano nje kabla ya kutolewa hukumu ya kesi ya unyanyasaji wa kijinsia inayomkabili.

Weinstein ambaye alikuwa mwigizaji nyota nchini Marekani, kabla ya kuwa mtayarishaji mwenye ushawishi mkubwa duniani, amepatikana na hatia ya mashtaka ya ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia na mahakama moja.

Kulingana na CNN, uamuzi huo ulifikiwa Jumatatu ya wiki hii na jaji wa Mahakama Kuu ya Jimbo la Manhattan, jijini New York.

Uamuzi huo ulitolewa baada ya mahakama kujadili kwa saa ishirini na sita.

Weinstein alishtakiwa kwa makosa mawili ya ubakaji, moja ya jinai na makosa mawili ya unyanyasaji wa kijinsia.

Mahakama ilimkuta Weinstein ana hatia kwa makosa mawili ya unyanyasaji wa kijinsia, na kumuondoa hatiani kwa wengine watatu.

CNN, imesema kwa sababu hakupatikana na hatia ya mashtaka ya kunyatia na kubaka, hivyo ilifanya iwe ngumu kwa mahakama kuhitimisha kesi.

Kutokana na makosa aliyepatikana na hatia, anaweza kukabiliwa na kifungo cha miaka ishirini na tano gerezani au angalau miaka mitano.

Hata hivyo jaji alimrudisha Harvey gerezani. Tarehe ya uamuzi wa mwisho imetajwa kuwa 20 Machi.

Orodha ya wanawake waliodai walishambuliwa na Weinstein ni pamoja na Angelina Jolie, Ashley Judd, Gwyneth Paltrow na Lupita Nyong'o ambaye alitoa ushahidi.

Lupita Nyong'o alisimulia jinsi alivyodhalilishwa kingono na Weinstein

Wakati akitoa mahojiano na New York Times, mshindi wa tuzo ya Oscar alielezea jinsi mtayarishaji huyo alivyombaka mara mbili.

Alisema aliamua kuongea baada ya kusikia wanawake wengine ambao walinyanyaswa na Weinstein wakitoa machungu yao.

Lupita aliendelea kutoa maelezo kamili ya jinsi shambulio la kwanza limetokea nyumbani kwake.

Akizungumzia juu ya kukutana kwake na Weinstein, alisema siku walipoonana alijaribu kukodi chumba baada ya kula chakula cha jioni na marafiki, lakini yeye alikataa.



# Mwingine Nollywood aaga dunia

TASNIA ya filamu nchini Nigeria inazidi kupata pigo baada ya mwigizaji na mtayarishaji mwingine mkongwe, Frank Dallas Ebulukwu, kuaga dunia.

Kwa kipindi kifupi tangu kuanza mwaka 2020, wasanii watatu wa Nollywood wamefariki jambo ambalo linazidisha simanzi kwa wadau filamu nchini humo.

Kulingana na taarifa ya msiba huo zilizotolewa na Ofisa Uhusiano wa chama cha waigizaji, Monalisa Chinda, mwili wa msanii huo utaagwa kwa siku tatu katika kanisa la FCT mjini Abuja, kabla ya kwenda kuzikwa nyumbani kwake.



## Naomi Campbell apamba mavazi

MBUNIFU wa Nigeria, Kenneth Ize, ameshiriki jukwaa la wiki la mavazi ya Paris kwa mafanikio.

Ize alikonga nyoyo za watu waliohudhuria baada ya nguo zake kuvaliwa na mwanamitindo maarufu Naomi Campbell.

Katika ukurasa wake, Kenneth Ize aliweka picha mbalimbali zikimuonesha mrembo huyo akipita jukwaani na nguo alizobuni na kushangiliwa kwa nguvu na watazamaji.

## Linda kweli wewe noma

MWIGIZAJI nyota kutoka Nollywood,Linda Osifo, ameonesha kwamba wasanii wa kike nao wapo juu, baada ya kuweka hadharani gari lake jipya aina ya Mercedes Benz.

Gari hilo la bei mbaya lina thamani ya pesa ya nchi hiyo Naira milioni 20, na kumfanya kuwa mwigizaji wa kike anayemiliki usafiri wa kifahari nchini humo.

Linda aliweka picha ya gari hilo katika ukurasa wake wa Instagram na kuwasababisha mashabiki wake kutoa pongezi kwa kupiga hatua.





## 2baba amtetea Wizkid

MWANAMUZIKI wa Nigeria, 2baba, amewawakia wale watu wanaowasema baadhi ya wasanii wanaolinda heshima zao.

Kulingana na mahojiano aliyofanya na chombo kimoja cha habari, 2baba amesema msanii mwenzake Wizkid, atabaki kuwa mkongwe kwa kizazi cha sasa.

Amesema nyota wote wanatafuta sehemu ambayo wanaweza kufurahia na kuwachukua vijana wenye vipaji na sio kujiona kama wanavyosema watu.

## Card B atangaza kutumbuiza tena Afrika


RAPA kutoka Marekani ambaye amejaa vituko, Cardi B, ambaye pia amejipachika jina la Chioma B, ametangaza kurudi tena Africa.

Cardi B amewataka mashabiki wake hasa wa bara la Afrika kumsubiri kwa hamu wakati atakaporudi tena kutoa burudani kabambe.

Card B ambaye alitangaza kuhamishia makazi yake nchini Nigeria, ametumia ukurasa wake wa Twiter kwamba mauzo ya tiketi ya tamasha atakalolifanya Afrika Kusini, yameanza kufanyika.



MAKALA



MIONZI YA SHERIA

# Ijue sheria ya utambuzi wa DNA kujua nasaba halali ya mtoto, ndugu

Na John Juma
0716217615

UTARATIBU wa wazazi kumjua mtoto nasaba yake kwa kutumia vipimo vya DNA upo kisheria na unakubalika. Hakuna sababu kuwepo na mivutano na migogoro kujua uhalisi wa mtoto.

Katika familia kumekuwapo na mivutano baina ya wazazi hasa mwanamume kujua kama mtoto husika ni wake au la kutokana kuwepo na shaka mbalimbali.

Kuna wanaopenda au ambao wangependa kufanya vipimo vya vinasaba(DNA) kuthibitisha kama ni wazazi kweli ama hapana. Basi utaratibu mzima huu hapa kutokana na Sheria ya Usimamizi wa Vinasaba vya Binadamu ya 2009,Sura ya 73.

**1. NANI ANAWEZA KUPIMWA DNA.**

Yeyote ambaye anahitaji kujua kuhusu uhalali wa uzazi wake anaweza kupima DNA. Upimaji huu hauna umri. Hata hivyo DNA si kwa jili ya masuala ya kuthbitisha uzazi tu, bali hutumika hata katika masuala ya ushahidi na upelelezi.

**2. NANI ANA MAMLAKA YA KUOMBA DNA KUPIMWA.**

Si kila mtu anaweza kuomba kupima DNA. Hata kama mwenye uhitaji ni wewe lakini bado huna mamlaka ya kuomba kupima DNA. Kifungu cha 25(2) cha Sheria niliyotaja hapo juu kinawataja wafuatao kuwa na mamlaka ya kuomba DNA kupimwa. Kinamtaja hakimu ambapo kuna kesi/shauri fulani linaendelea, Wakili, ofisa ustawi wa jamii, ofisa polisi mwenye cheo zaidi ya Inspekta, daktari na mkuu wa wilaya.Hawa ndio wenye mamlaka kuomba.

Kwahiyo wewe ukiwa na shida ya DNA unaweza kumuona mmoja kati ya hawa ili aandae maombi ya kupima DNA na kuyapeleka kunakostahili.

**3.MAOMBI YA DNA YANAPELEKWA WAPI.**

Kifungu cha 24 cha Sheria ya Usimamizi wa Vinasaba kinaitaja maabara ya Vinasaba vya binadamu ya Mkemia Mkuu wa serikali kuwa na Mamlaka ya kupima DNA. Pia kinazitaja na maabara nyingine ambazo zitakuwa na leseni maalum ya kupima DNA kuwa na mamlaka hayo.

Kwahiyo maombi ya DNA yatapelekwa moja kati ya sehemu hizo mbili.

**4.NANI ANAPELEKA MAOMBI NA KUFUATILIA MAJIBU.**

Wahusika waliopimwa DNA(sample source) hawaruhusiwi kupeleka wala kufuatilia majibu ya DNA. Maombi na Majibu ya DNA yatapelekwa na kufuatiliwa na hao niliowajataja hapo juu katika 2 ambao ndio wenye mamlaka ya kuomba DNA kupimwa.

Hawa ndio watapeleka maombi na ndio watachukua majibu na kuwasomea wahusika.

**5. MAOMBI YA KUPIMA DNA YANAKUWAJE?.**

Kifungu cha 26(1) cha Sheria hiyo kinasema maombi ya kuomba DNA kupimwa yatakuwa katika mfumo maalum wa maandishi. Yataeleza muombaji na cheo chake, yataeleza wanaotakiwa kupimwa DNA na sahihi zao,yataeleza DNA ipimwe katika nini na nini, yataeleza sababu za kupima DNA,yatakuwa na kiapo kuwa majibu hayatatumika kwa shughuli nyingine tofauti na iliyoombwa, na yatasainiwa na muombaji ambaye ni wale niliowataja katika 2 juu.

**6. ADA YA KUPIMA DNA NI KIASI GANI.**

Malipo yapo. Na mpaka desemba 2018 makala haya yalipoandikwa ada ni Tshs 100,000/=( laki moja tu) kwa kila mtu. Kawaida DNA ya kutambua uzazi(parentage) hupimwa watu watatu. Mama, baba na mtoto. Kwahiyo kila mmoja ni laki moja na hivyo watatu ni laki tatu.

Nani anatoa hiyo hela, anaweza kuwa yule anayehitaji kuthibitisha kwamba yeye ni mzazi halali, au yakawa ni maelewano ya wahusika, au kutokana na maelekezo ya mahakama.

**7. DNA INAPIMWA KATIKA NINI NA NINI.**

Kifungu cha 29(1) cha sheria hiyo kinaeleza maeneo ambayo DNA inaweza kupimwa kuwa ni kwenye mate, damu, mkojo, ute ute wa sehemu za siri, nywele, haja kubwa, ngozi, mifupa, meno, mbegu za kiume, unyayo na sehemu nyingine ambayo mhusika atakuwa amegusa, kukanyaga au kuwapo au alama yoyote ya uwepo wake.

**Kwa msaada wa mtandao**



KALAMU YA MWALIMU

# Shule ya Sekondari Bunge ni alama ya utaifa, mshikamano na uthubutu

Na Reubeni Lumbagala

KUTOKANA na mila potofu za baadhi ya jamii, mtoto wakike amekuwa akibaguliwa katika kupata haki muhimu ya elimu ambayo ni msingi na msaada mkubwa kwa maisha yake ya sasa na ya baadaye.

Kutokana na hali hii, serikali kwa kushirikiana na asasi na taasisi zisizo za kiserikali wamekuwa wakifanya juhudi kubwa kuhakikisha mtoto wa kike anapata haki ya elimu bila kikwazo chochote.

Katika jitihada hizo, wamekuwa wakijenga shule za sekondari za wasichana ili kuongeza wigo wa usajili ili waweze kupata fursa ya elimu ambayo ni nguzo muhimu kwa mustakabali mwema wa maendeleo ya wanawake. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama mdau muhimu wa maendeleo ya elimu hapa nchini, wamechukua hatua ya kuweka alama isiyofutika katika nyanja ya elimu kwa kujenga shule ya mfano jijini Dodoma.

Shule hiyo maalum kwa wasichana ambayo itakapokamilika itajulikana kwa jina Shule ya Sekondari ya Wasichana Bunge.

Shughuli za ujenzi wa shule hiyo unaendelea ambapo Februari 25 mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tamisemi, Selemani Jafo alitembelea eneo hilo la ambako ujenzi unafanyika.

Lengo la Spika Ndugai kwenda na Waziri Jafo katika eneo la mradi hilo ni kumwezesha kufahamu maendeleo ya mradi ili kupata maboresho na ushauri.

Spika Ndugai alisema “Hapa tunajenga kwa kutumia‘Force Account’ mfumo ule ule unaosisiwa na Tamisemi na ramani za majengo ni zile zile za Tamisemi ila kuna baadhi ya maeneo tumeboresha kidogo.Hatujaenda nje ya maelekezo ya Wizara hii kuhusu ujenzi wa miundombinu ya shule”.

Ni jambo jema kuona mhimili wa bunge ulivyochukua hatua za kuchagiza maendeleo ya elimu hasa kumsaidia mtoto wa kike ambaye anakabiliwa na changamoto nyingi.

Fedha za ujenzi wa shule hii zimepatikana baada ya wabunge kuchangisha kupitia matukio ya kijamii.

Jumla ya shilingi bilioni1.2, zimepatikana kutoka katika sehemu ya posho za wabunge na michango ya wadau hao.

Wakiwa katika eneo hilo la mradi, Waziri Jafo amesema amefarijika kwa kuona mradi huo muhimu kwa maendeleo ya nchi.

“Nimefarijika sana kuona wazo hili limeanza kutimia na ndoto za Bunge sasa zinanza kutimia. Mimi nitapita mara kwa mara kuangalia maendeleo ya ujenzi huu”. Amesisitiza.

Kukamilika kwa shule hii kutatoa fursa kwa wanafunzi wa kike kutoka maeneo mbalimbali ya nchi kupata nafasi ya kujiunga kidato cha tano na sita.

Hii ni fursa adhimu ambayo watoto wa kike wanapaswa kuichangamkia ili kuingia katika historia ya kusoma katika shule iliyojengwa kwa wazo na michango ya wabunge.

Ikumbukwe kuwa, kabla ya wazo la kujenga shule hii, wabunge walipanga kutumia fedha hizo katika ujenzi wa vyoo vya mfano ya wasichana katika majimbo yote nchini, lakini baadaye waliamua kubadili wazo hilo na kuamua kujenga shule katika makao makuu ya nchi.

Ubunifu huu wa wabunge umeonyesha namna taasisi mbalimbali zinavyoweza kuchangia shughuli za maendeleo nje ya mikakati yao ya kawaida ya kazi.

Haikutarajia kama bunge lingeweza kujenga kujenga shule ya kisasa kwa ajili yawatoto wa kike.

Ajenda ya elimu ni ya kitaifa ambayo wadau wote wanapaswa kuiunga mkono kwa kusaidia kwa mawazo na vifaa ili kufanikisha ujenzi

Shule ya Wasichana ya Bunge ni taasisi muhimu katika kuchagiza kufikiwa kwa dira ya Taifa ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Wale wote watakopata fursa ya kusoma katika shule hii wasome kwa bidii, wasiwaangushe wabunge na wadau wengine waliosaidia ujenzi wa shule hiyo. Tafakari.

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.**
**Maoni: (+255) 765 409249.**

MAKALA

# Juhudi zaidi zinahitajika ulaji virutubisho

**Na Gaudensia Mngumi**



WANAWAKE na watoto wa Tanzania pengine na kwingineko duniani, ndiyo waathirika wakubwa wa matatizo ya utapiamlo na lishe duni. Watoto wa chini ya miaka mitano ni wahanga wa ukosefu wa lishe bora na ndiyo wenye udumavu, ukosefu wa madini ya chuma unaoleta upungufu wa damu.

Watoto pia pamoja na lishe duni wanakabiliwa na matatizo ya kukosa foliki asid na kupelekea ulemavu wa vichwa vikubwa na mgongo wazi, pia wanaelezwa kuwa wana upungufu mkubwa wa madini ya chuma, vitamin A, B 12 na madini joto.

Kwa mujibu wa taarifa za Mpango Mkakati kwa Tanzania unaondaliwa na Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa Tanzania wa mwaka 2017-2021, utapiamlo na udumavu unaathiri asilimia 34 ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano nchini na kwamba athari ni za kiwango cha juu mno.

Uhaba mkubwa wa chuma, madini joto na vitamin A unaonekana kwa kinamama na watoto, lakini ukosefu wa chuma unachangia ongezeko la tatizo la anemia (upungufu wa damu) kwa kundi hilo.

Udumavu na lishe duni una athari kubwa kwa maisha ya watoto kwani unaathiri utaratibu mzima wa ukuaji wa mwili, akili na uwezo wa ubongo kufanyakazi . Si hivyo tu unaathiri uchumi wa nchi na taifa linalotegemea watoto kukua na kuwa nguvu kazi.

Kwa kuliona hilo Mpango wa Chakula Duniani, unashirikiana na serikali na wadau wa lishe kwenye kuhudumia jamii zilizoathirika na udumavu na lishe duni katika wilaya za Bahi na Chamwino mkoani Dodoma pamoja na Singida Vijijini na Ikungu za mkoani Singida.

Mpango huo wa WFP unasema wanufaika huhudumiwa kwa kupatiwa vyakula vyenye virutubisho na kuelekezwa namna ya kuandaa mlo kamili wenye vyakula vya aina zote kwa kutumia vyakula vya aina mbalimbali vinavyopatikana kwenye jamii hizo. Lengo ni kupunguza gharama na kufanikisha upatikanaji.

"Watoto wadogo, wajawazito na kinamama wanaonyonyesha wanapatiwa vyakula vyenye virutubisho ili kuwaepusha na utapiamlo na lishe duni."Inasema ripoti ya WFP na kwamba katika utaratibu huo kina mama wajawazito, wanaonyonyesha na watoto wenye umri wa miezi sita hadi 23 wanapata vyakula vya wanga vilivyochanganywa na virutubisho muhimu kila mwezi kwa lengo la kulinda maisha ya watoto hasa kwenye siku 1,000 za maisha ya watoto wadogo.

Aidha, mpango huo, unawafundisha na kuwahamasisha kinamama kuwalisha watoto vyakula vyenye virutubisho na lishe bora vinavyopatikana sehemu wanazoishi na kuendeleza ulaji huo ndani ya jamii, andiko la WFP linaongeza.

**KUTIBU UTAPIAMLO**

Aidha, WFP inasema watoto walio na utapiamlo wenye umri wa kuanzia miezi sita hadi 59 wanapata lishe bora na maalumu kila mwezi yenye nafaka zilizowekewa virutubisho pamoja na mafuta yaliyoongezewa virutubisho, na pia vitamin A na D.

**WANUFAIKA WENGINE**

Wananchi wengine wahitaji wa lishe bora na taarifa za namna ya kuandaa na kula chakula bora wanahudumiwa kupitia uhamasishaji na uwezeshaji wananchi kwenye kufuga na kulima mazao mchanganyiko ili kupata lishe bora, ya kutosha pia kuwahimiza wanavijiji kuweka akiba kwa ajili ya kumudu mahitaji mbalimbali ikiwamo chakula na mitaji ya biashara.

Pamoja na jitihada za WFP, serikali imetangaza mpango mkakati wa kuhakikisha kila mtoto chini ya miaka mitano anapata virutubisho ili kupunguza udumavu kwa watoto.

Virutubisho vinavyotarajiwa kuongezwa vitawekwa kwenye mafuta ya kula, nafaka kama unga wa ngano na sembe wakati wa kusaga nafaka hizo.

Mpango mwingine ni wa kushirikiana na wadau wa kilimo kuhamasisha kilimo na matumizi ya mazao yaliyoongezwa virutubisho kama viazi lishe na mahindi lishe yenye rangi ya njano ambayo yana kiwango kikubwa cha vitamin A na maharage yenye vitamini, madini, chuma na zinki.

Mkakati huo unatekelezwa na Taasisi ya Chakula la Lishe (TFNC), kwa lengo la kupunguza udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka asilimia 32 zilizopo sasa hadi kufika chini ya asilimia 20, anayaeleza hayo Mkurugenzi Mtendaji wa TFNC, Dk. Germana Leyna, anapozungumza na wanahabari.

Aidha, anasema lengo ni kupunguza utapiamlo kutoka asilimia 3.5 za sasa hadi chini ya hapo na kutokomeza tatizo la upungufu wa damu kwa wajawazito ambalo sasa ni asilimia 29, ikimaanisha kuwa kila wanawake 100 wajawazito, 29 wana tatizo la anemia.

Dokta Leyna anasema, "Kwa kushirikiana na sekta binafsi tumetekeleza kanuni za kuongeza virutubisho kwenye chakula. Lengo letu ni kumaliza tatizo la udumavu utapiamlo kwa watoto wa chini ya miaka mitano,"

Anasema wanaongeza virutubisho vya vitamin A kwenye mafuta ya kula, vitamin B 12, madini ya zinki, foliki aside na madini chuma kwenye unga wa ngano na mahindi.

Dk. Leyna, anasema pia wanashirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wazalishaji wadogo wa chumvi na viwanda vidogo vya kuzalisha bidhaa zinazoongezewa madini joto (iodine).

**VIRUTUBISHO MUHIMU**

Kwa ujumla virutubisho vinavyoongezwa katika vyakula ni muhimu hii ni kutokana na jukumu kubwa vilivyonavyo mwilini, kwa mfano vitamin A ni muhimu kuongeza na kuimarisha kinga ya mwili.

Jamii hii ya virutubisho inapatikana kwenye vyakula mfano maboga, maembe na vyakula vyote vyenye rangi ya njano.

Madini ya zinc yanayoongezwa kwenye unga ni muhimu kwani yanaimarisha mifumo ya uzazi ya wanawake na wanaume na kutibu tatizo la ugumba. Kwa wanawake husaidia kuweka uwiano sawia 'balansi' wa homoni na ukuaji wa mayai. Kwa wanaume huongeza uzalishaji wa mbegu na kuongeza hamu ya tendo la ndoa.

Chuma (iron) ni muhimu kwani ukosefu wa madini hayo unamaanisha upungufu wa damu kwa kuwa ndicho chanzo cha mwili kuzalisha damu.

Watoto na wajawazito wanaweza kuugua anemia kutokana na ukosefu wa damu mwilini . Changamoto za kukosa damu huchangiwa na maradhi ya malaria au minyoo.

Kwa ujumla ukosefu wa madini aina iron unaweza kusababisha ulemavu na matatizo ya kiakili miongoni mwa watoto wachanga na wadogo. Ukosefu wa damu mwilini ndilo tatizo linalochangia kwa kiasi kikubwa vifo vya wazazi nchini.

Vitamin B12 ndiyo inayoongeza protini mwilini na pia inaboresha uwezo wa mwili kujilimbikizia protini muhimu.

Aidha vitamin B12 inahusika katika mfumo wa kinga, huboresha na kuimarisha uwezo wa chembe zinazohusika na kinga ' lukosaiti'. Kwa ujumla ni muhimu katika mchakato wa damu na hupunguza shinikizo la damu.

**UELEWA WA VIRUTUBISHO.**

Katika jitihada za kufahamu hali ya uelewa wa masuala ya lishe na matumizi ya vyakula vyenye virutubisho, Nipashe ilitembelea baadhi ya mamalishe katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kampuni zinazoandaa chakula kwenye migahawa ya wanafunzi (kafteria).Katika eneo la mama lishe wanaoandaa vyakule eneo la Polisi chuoni hapo, Zeituni Majabele na Sikujua Mohamed, wanaeleza kuwa hawafahamu habari za kuandaa vyakula vyenye virutubisho na TFNC haijawahi kuwafikia.

Licha ya kwamba mamalishe hao wanahudumia kundi kubwa la wanafunzi na wana wateja wengi, wanakiri kuwa wanaandaa unga wa dona wenyewe na pia wananunua sembe kutoka kwa wazalishaji bila kufahamu umuhimu wa kutumia unga ulioongezewa virutubisho.

Kinamama hao wanaeleza kuwa wananunua unga wa ngano kwa ajili ya kuandaa vitafunio lakini hawafahamu kuhusu uwepo wa unga ulioongezewa virutubisho hivyo.Aidha, kwa upande wa kampuni inayoandaa chakula kwenye mgahawa (kafteria) ya Harvard Chuo Kikuu, maofisa wa ununuzi na utayarishaji vyakula nao wanaeleza kuwa hawajafahamishwa kuhusu matumizi ya vyakula vyenye virutubisho.

Unga wa sembe na dona ambao haujaongezewa virutubisho na kwamba licha ya kuwa wadau muhimu wanaolisha jumuiya kubwa ya wanafunzi hawajakutana na maofisa wa TFNC kuwaelezea kuhusu kuandaa vyakula vyenye virutubisho. Kwa kuangalia maelezo yao ni muhimu TFNC na wadau wa lishe wakafikisha ujumbe wa umuhimu wa kutumia virutubisho na umuhimu wa kutumia vyakula vilivyoongezewa virutubisho na pia kuwahimiza kuandaa lishe na mlo bora kwa kutumia vyakula vinavyopatikana katika maeneo yao.



MAKALA

# Hamahama ya wanasiasa yamwibua Ngawaiya

Na Sabato Kasika

UCHAGUZI mkuu unatarajiwa kufanyika ndani ya mwaka huu, wananchi watapata fursa ya kuchagua viongozi wao akiwamo rais, wabunge na madiwani.

Kulingana na taratibu ambazo imezoeleka, uchaguzi mkuu hufanyika kila mwisho mwezi wa Oktoba kila baada ya miaka mitano.

Katika kipindi hicho vyama vya kisiasa vinanadi sera zao kupitia wagombea waliowateua kwa lengo la kuwashawishi wapiga kura kuvichagua.

Wakati Watanzania wakiajinadaa, ni vyema kujikumbusha kile kilichojitokeza kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Katika muda kama huo kulishuhudiwa hamahama ya wanasiasa kutoka chama kimoja kwenda kingine.

Mtindo huo wa baadhi ya wanasiasa kuhama wakati wa kuelekea kwenye uchaguzi, umekuwa ni jambo la kawaida, kutokana na ukweli kwamba hawabanwi na sheria yoyote kufanya hivyo.

Wimbi la kuhama kwa wanasiasa mwaka 2015 lilivitikiswa vyama vikubwa ikiwamo CCM na Chadema, lakini inaelezwa kuwa tangu serikali ya awamu ya tano iingie madarakani, hali imekuwa tofauti kidogo.

Katika mahojiano na gazeti hili, mwanasiasa mkongwe, Thomas Ngawaiya, anasema hali ilivyo sasa vyama vya upinzani vitarajie kukumbwa na wimbi la aina hiyo hasa kukimbiwa na wanachama.

Ngawaiya, anasema sasa ni kutesa kwa zamu, wapinzani walitesa mwaka 2015 kwa kuchukua idadi kubwa ya makada wenye majina ndani ya CCM, lakini hilo halitarajii kutokea mwaka huu.

Matukio ya kuhama kwa wanasiasa kutoka upinzani kwenda CCM kuanzia mwaka 2016 ni dalili kwamba itaendelea hadi wakati nchi ikielekea kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Anasema, safari hii inaonekana vyama vya upinzani ndivyo vinaendelea kulizwa zaidi, kutokana na wanachama na viongozi wake kukimbilia CCM, kutokana na kile wanachodai kuwa ni kuridhishwa na utendaji wa serikali.

"Ni kweli kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 vyama vilitikiswa na hamahama ikiwamo CCM, kwa sababu mgombea urais wa chama tawala alikuwa mpya, hivyo baadhi walidhani atawaangusha," anasema Ngawaiya.

Anasema, wanasiasa kama yeye na wengine, hawayumbi, kwa vile walijua kuwa ni chaguo sahihi na sasa anafanya mambo makubwa na kusababisha wale waliokimbia wakati huo kurudi.



Thomas Ngawaiya

Anasema, kama rais Dk. John Magufuli angekuwa anamaliza muda wake, hamahama ya wanasiasa kutoka pande zote ingeweza kujirudia, lakini kwa sasa haamini kama inaweza kuwa hivyo.

"Watanzania na wanasiasa kwa ujumla wameshaona utendaji wa rais wetu, hivyo sidhani kwamba wanaweza kuhama badala yake watamuunga mkono amalizie muda wake wa miaka mitano ijayo," anasema.

Ngawaiya anasema, kama itatokea wakawepo wa kuhama toka CCM kwenda upinzani, idadi itakuwa ni ndogo siyo kama ilivyokuwa mwaka 2015.

"Maoni yangu kama ni safari ya kutoka Dar es Salaam kwenda Kilimanjaro, basi rais amesafiri vizuri na kufika katikati ambako ni Korogwe, hivyo kuna haja ya kuachwa amalizie safari yake," anasema.

**UROHO WA MADARAKA**

Mwanasiasa huyo ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), anasema, yawezekana wapo watakaohama kwa sababu ya uroho wa madaraka, hao lazima watazamwe.

"Kwanza hakuna anayezuiwa kuhama chama, na inawezekana wapo wanaosubiri wakose nafasi za uongozi kwenye kura za maoni katika vyama vyao ndipo wahame, hao ni waaroho wa madaraka," anaonya.

Anasema anaamini waliohama upinzani na kwenda CCM, walifanya hivyo kwa lengo la kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano katika kuleta maendeleo, siyo kwa ajili kutafuta vyeo.

"Wakifanya hivyo watakuwa wanajisumbua tu kwa sababu sheria mpya ya vyama vya siasa inataka mtu anapohama kutoka chama kimoja kwenda kingine ni lazima atimize mwaka mmoja kwanza ndipo awanie uongozi," anasema.

Anasema, wanasiasa wenye malengo hayo itakuwa imekula kwao kwa vile sheria ikishapitishwa ni lazima itekelezwe.

Katika hamahama ya wanasiasa vyama vya Chadema, CUF na ACT Wazalendo ndivyo vimeathirika kutokana na wanachama wao wengi kujiunga na CCM.

Kwa maoni ya Ngawaiya ana uhakika pigo hilo litazidi kabla ya uchaguzi mkuu.

"Kuna wabunge wabunge wanasubiri kumaliza muda wao ili wahame huko, ninaaamini kwamba CCM itaendelea kuvuna wanachama wapya zaidi kutoka katika vyama hivyo vikubwa," anasema.

Ngawaiye ambaye amewahi kuwa mbunge wa Moshi Vijijini kwa miaka mitano, anasema, yeye ni miongoni mwa watu wanaounga mkono mambo ya maendeleo yanayofanywa na chama tawala.

# Corona yazidi kuleta taharuki duniani....

## ■Saudi Arabia yazuia hija, Iran vifo vyaongezeka, Afrika yajiandaa



DUNIA inatikiswa na kuibuka kwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona. Mataifa mbalimbali yanahangaika kukabiliana na ugonjwa huo huku baadhi yakiendelea kushuhudia athari kubwa inayotokana na Corona.

Toka virusi vya corona viripotiwe mwezi Desemba mwaka jana, zaidi ya watu 80,000 kutoka nchi 40 tayari wameshaambukizwa virusi hivyo. Wengi wao wakiwa nchini China ambako ugonjwa huo ulipoanzia.

Iran ambayo ndio nchi pekee nje ya China ambayo imeripoti vifo vingi, baada ya watu 19 kupoteza maisha na wengine 139 kupata maambukizi.

Hali hiyo inawafanya madaktari wa magonjwa ya kuambukiza kuhofia kuwa nchi hiyo inaweza kuwa na wagonjwa wengi, lakini inaficha ukweli.

Katika Bara la Ulaya hali ni mbaya zaidi, hasa nchini Italia ambako mpaka sasa watu 400 wamethibitika kuambukizwa kutoka idadi ya watu 80 ya awali.

Watu 12 tayari wameshafariki nchini humo kutokana na mlipuko huo.

**SAUDI ARABIA YACHUKUA HATUA**

Serikali ya Saudi Arabia imechukua hatua ya kuzuia wageni wote wanaoingia nchini humo kwa safari za kidini, ikiwamo wanaotembelea miji mitakatifu ya Kiislamu ya Makka na Madina.

Mamilioni ya watu huingia Saudia mwaka mzima kufanya ibada ya Umra, na wengi zaidi huingia kwa pamoja kufanya ibada ya Hija.

Tofauti na Hija, Umra ambayo hufahamika kama Hija ndogo, hufanyika katika kipindi chochote cha mwaka.

Marufuku hiyo inawalenga mahujaji raia wa nchi za nje ambao wanakwenda huko kuitekeleza ibada zao.

Haijafahamika kama ibada ya Hija ya mwaka huu ambayo inatarajiwa kuanza mwishoni mwa Julai inaweza kuathirika kutokana na hofu ya kusambaa kwa virusi vya corona duniani.

Mpaka sasa Saudia bado haina mtu ambaye amethibitika kuambukizwa virusi hivyo.

Makka ndio mji ambao Mtume Muhammad alipozaliwa, na kuna msikiti mtakatifu zaidi. Madina ndipo alipofariki na kuzikwa.

Saudi Arabia imeeleza kuwa toka mwezi Oktoba imetoa viza zaidi ya 400,000 za watalii kutoka nchi mbali mbali duniani.

**DUNIA IJIANDAE KWA JANGA**

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), dunia inapaswa kujiandaa kwa uwezekano wa janga la virusi vya corona.

WHO imejiuzia kuuita mlipuko wa virusi hivyo kuwa janga la Dunia, lakini imetahadharisha nchi zinapaswa kuwa katika maandalizi.

Ugonjwa hadi utangazwe kuwa janga ni pale maambukizi yake yanaposambaa kwa urahisi kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine katika maeneo mengi ya dunia.

Mpaka sasa zaidi ya watu 2,700 wameshafariki dunia kutokana na ugonjwa wa Covid-19.

**AFRIKA JOTO LINAPANDA**

Afrika ambayo inaelezwa kwamba ina miundombinu dhaifu ya afya, imeripotiwa nchi mbili mpaka sasa zimethibitisha kuingia kwa ugonjwa huo.

Nchi hizo ni Algeria na Misri kila moja imeripoti mgonjwa mmoja.

Shirika la afya ulimwenguni, WHO kanda ya Afrika Mashariki, limesema kuwa mataifa ya ukanda huo yamejiandaa kudhibiti mlipuko wa virusi hivyo.

Ofisa wa kisayansi wa HYPERLINK "https://www.who.int/" \o "Shirika la afya ulimwenguni (Wavuti kwa lugha ya kiingereza)" \t "_blank" WHO kwa nchi za Afrika Mashariki, Dkt. Peter Borus, mwenye makazi yake jijini Nairobi nchini Kenya, amesema katika mahojiano yake na UN News Kiswahili kwamba maandalizi yamefanyika na wameridhika.

"Kwa maandalizi kuna vifaa na serikali ikiwa inaongoza kwa hii juhudi inashirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo WHO." Anasema.

Ofisa huyo amesema serikali za nchi hizo zimejiandaa kwa vifaa vya kujikinga na kufanya uratabi maalum katika maeneo yanayoingia wageni kuanzia bandarini, mipakani na viwanja vya ndege.

"Wamejitayarisha kabisa, ukiona vile wanafanya kazi kwenye viwanja vya ndege na bandarini na kwingineko ambako watu wanaweza kujitokezea na hizo dalili za virusi hivyo. unaona kabisa nchi zimejitayarisha," anasisitiza.

Virusi vya Corona viliibuka nchini China na HYPERLINK "https://news.un.org/sw/story/2020/01/1080522" kutangazwa kuwa dharura ya afya ya umma duniani tarehe 30 mwezi wa Januari.



## Papa Francis augua mafua, apunguza shughuli zake

**VATICAN,** Roma

KIONGOZI wa kanisa Katoliki duniani, Papa Francis, ameahirisha utaratibu wake wa kila Ijumaa wa kutoa baraka kwa waumini kutokana na kuumwa mafua.

Ofisi ya Vatican imesema kuwa Papa Francis, mwenye umri wa miaka 83, aliadhimisha ibada ya misa kama kawaida jana asubuhi na kusalimiana na waumini mwishoni.

Alipanga kuendelea na mikutano yake binafsi kama kawaida, lakini aliamua kuahirisha kukutana na waumini. Hata hivyo, Vatican haijasema nini kinachomsumbua Papa Francis, lakini alikuwa na kikohozi kikali wakati wa ibada ya misa ya Jumatano ya Majivu, wiki hii.

Jana kiongozi huyo aliahirisha ziara yake iliyokuwa imepangwa kuzunguka mji huo kuadhimisha ibada ya misa na mapadri wa Roma. **DW**

# Uturuki yalipa kisasi, vita kamili yanukia

**ANKARA,** Uturuki

UTURUKI imeanza kulipiza kisasi baada ya askari wake 33 kuuawa katika mashambulio ya anga yaliyofanywa na vikosi vya Syria.

Idadi kubwa ya askari wamejeruhiwa katika mashambulizi hayo yaliyofanyika katika jimbo la Idlib, amesema Rahmi Dogan, ambaye ni gavana wa jimbo la Hatay la Uturuki.

Hata hivyo, taarifa nyingine zinasema idadi ya vifo ni kubwa.

Uturuki imejibu kwa kuyalenga na kushambulia maeneo ya vikosi vya Syria.

Vikosi vya Syria vinavyoungwa mkono na Urusi vinajaribu kurejesha jimbo la Idlib ambalo kwa sasa linadhibitiwa na waasi wanaosaidiwa na wanajeshi wa Uturuki.

Maofisa nchini Syria bado hawajatoa kauli yao kuhusu mapigano ya sasa ya Idlib, jimbo la mwisho lililosalia mikononi mwa upinzani.

**Urusi pia imeishutumu Uturuki kwa kukiuka makubaliano ya mwaka 2018 ya usitishaji mapigano kwa kuwaunga mkono waasi kwa kufyatua makombora.**

Jeshi la Uturuki lilianza kupiga maeneo ya Syria baada ya Rais wa nchi hiyo, Recep Tayyip Erdogan, kumaliza mkutano na maafisa wa ngazi ya juu wa usalama mjini Ankara.

Kiongozi huyo wa Uturuki anataka vikosi vya Syria virudi nyuma kutoka kwenye maeneo ambayo nchi hiyo imeweka vituo vya uchunguzi.

Lakini serikali ya Syria na Urusi zimekataa madai yake ya kurudi nyuma kwenye mistari ya usitishaji mapigano iliyokubaliwa mwaka 2018.

Urusi pia imeishutumu Uturuki kwa kukiuka makubaliano ya mwaka 2018 ya usitishaji mapigano kwa kuwaunga mkono waasi kwa kufyatua makombora.

Waangalizi wa haki za binadamu nchini Syria wenye makao yao makuu nchini Uingereza,The UK-based monitor, the Syrian Observatory for Human Rights, wamesema kuwa wanajeshi 34 wa Uturuki waliuawa Alhamisi katika mashambulio ya anga jana jioni.

Waliojeruhiwa wamerudishwa nchini mwao kwa ajili ya matibabu, amesema Bw. Dogan.

"Yote yanajulikana maeneo ya serikali ya Syria yalishambuliwa na ndege za Uturuki na vikosi vya ardhini," Mkurugenzi wa mawasiliano wa Uturuki Fahrettin alinukuliwa na Shirika la habari la taifa Anadolu akisema na kuongeza "Uturuki imeamua kujibu kwa ukarimu mashambulio,"

Wakati huo huo ,Uturuki ambaye ni mjumbe wa Muungano wa kujihami wa nchi za Magharibi Nato imesema waziri wake wa mambo ya nje Mevlut Cavusoglu amezungumza na katibu mkuu wa muungano wa Nato -General Jens Stoltenberg.

Uwanja sasa umewekwa tayari kwa ajili ya mapambano kamili baina ya Uturuki na Syria.

Inaonekana Rais Bashar al-Assad ameazimia kuchukua tena udhibiti wa eneo hilo, na Urusi tayari inaunga mkono mkakati huo. **BBC**



Wakazi wa mji wa New Delhi nchini India, wakirejea katika makazi yao baada ya maandamano yaliyoibua ghasia kupinga sheria mpya ya uraia. **PICHA: AFP**

# Nigeria yathibitisha mgonjwa wa Corona

**ABUJA,** Nigeria

NCHI ya Nigeria imethibitisha kuwapo kwa mtu mmoja mwenye maambukizi ya virusi vya corona.

Mgonjwa huyo, raia wa Italia anayefanya kazi nchini Nigeria, alisafiri kwa ndege kwenda mji wa kibiashara wa Lagos akitokea Milan Februari 25 mwaka huu.

Mamlaka zinasema mgonjwa huyo anaendelea vizuri na hakuna dalili ya hatari wakati anapatiwa matibabu katika hospitali ya jijini Lagos.

Serikali ya Nigeria imesema ilijiandaa kukabiliana na tukio lolote, pia imekuwa ikiandaa vituo kwa ajili ya operesheni za dharura, ili kuchukua hatua za udhibiti.

Mamlaka zimesema zimeanza kuwatambua wale wote waliokaribiana naye tangu aliporejea Nigeria. Zaidi ya watu 80,000 wameripotiwa kuathirika katika nchi 40.

Zaidi ya watu 60 wamepoteza maisha nje ya China, ambapo mlipuko ulipoanza. Hatahivyo, idadi ya maambukizi nchini China imeendelea kushuka.

Wakati huo huo, Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa ameamuru kuondolewa kwa raia wa Afrika Kusini 132 wanaoishi mjini Wuhan.

Uamuzi ulitangazwa siku ya Alhamisi baada ya kikao cha baraza la mawaziri, kufuatia maombi ya wana familia wa raia hao wanaoishi Wuhan.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka ofisi ya rais imeeleza utafanyika lakini haikueleza ni lini wataondolewa huko. Serikali imesema raia 132 kati ya 199 wanaishi mjini Wuhan wameomba warejee nyumbani.

Hakuna aliyegundulika kuathirika na virusi au kuwa na dalili za ugonjwa, lakini wakiwasili nchini humo watawekwa kwenye karantini kwa siku 21kama hatua ya tahadhari.

"Serikali imekuwa ikifanya mazungumzo na familia za walioathirika wakati idara zinazohusika zikifanya mipango muhimu kuwapokea," iliongeza taarifa hiyo.

Jeshi na wataalamu wa afya watatoa msaada wakati watakapokuwa wanawekwa karantini. Shirika la ndege la Afrika Kusini, zimesitisha safari za moja kwa moja kwenda China.

Nchi zingine za Afrika zilizothibitisha kuwa na wagonjwa wa Corona ni Algeria na Misri. **BBC**

# HADITHI


ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# MAUAJI HARUSINI-2

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**




**Na Adam Fungamwango**

"Sawa Bosi, lakini hapa ni lazima tukubaliane, eneo sahihi la kufanya mauaji ni wapi? Wakati wanatoka Kanisani? Njiani wakati wapo kwenye gari, au nyumbani kwa bwana harusi wakati wanawasili?" Mmoja aliyekuwa kwenye kikao hicho akauliza.

"Mimi nadhani swali hilo tungemtupia Tamim alijibu kwa sababu mimi binafsi ninachohitaji bwana harusi na bibi harusi wauawe tu basi. Sijali wauawe vipi au wauawe wapi. Ninachohitaji wasiwepo kwenye uso wa dunia." Aliunguruma bosi.

"Mimi nadhani, sehemu ambayo itakuwa rahisi sana kuwaua wote wawili ni pale watakapokuwa wanashuka kwenye gari lao, wakipokelewa na ndugu zao, kuelekea sehemu ambayo wameitenga kwa sherehe au kuelekea kuingia nyumbani kwao. Hiyo ni sehemu ambayo mara nyingi inakuwa si tulivu, kunakuwa na pilikapilika na shamrashamra ya ngoma na mbwembwe nyingi, kwa hiyo kunakuwa hakuna utulivu, au watu wanaofuatilia jambo lingine zaidi ya kuwaona maharusi." Tamim alitoa msimamo wake kutokana na uzoefu wa kazi yake hiyo kutokana na kuifanya kazi hiyo ya kuua watu kwenye sehemu tofauti na mazingira tofauti pia.

"Bwana Tofiki, hakikisha gari letu linakuwa moja kati ya magari ya mbele kwenye msafara wa harusi ili kazi yetu isiwe ngumu sana. Na hakikisha, wakati muda ukiwadia wa kufanya mauaji, basi hakikisha gari liwe limeshatoka eneo la magari mengine yaliyo kwenye msafara na kukaa kwenye eneo sahihi pekee ambalo mambo yakishamalizika, basi gari haraka sana linaondoka na kwa ninavyokujua kuwa ni mtaalam wa kuendesha magari kwa kasi, hata wakikufukuza na pikipiki ya polisi hawawezi kutupata."

**Kwa kutumia pesa zake na ushawishi aliweza kuwapata vijana wanne wanaoweza kufanya vitu tofauti, lakini lengo likiwa ni moja tu, Grace na Patiyo watoweke duniani kwa sababu hawana adabu.**

"Bwana Tamim, kila mtu na utaalamu wake, wewe ukishamaliza kula vichwa, hayo mambo ya kutambaa na gari niachie mimi." Tofiki, ambaye mtaalam wa kuendesha gari kwa kasi, na alishawahi kuwa mshindi wa mbio za magari miaka mitatu iliyopita, alijisifu mbele ya wenzake.

Tahadhari kubwa ilikuwa imechukuliwa wakati wa kuandaa mkutano huo. Wajumbe hao wanne waliingia kwa siri katika eneo hilo vilitegwa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuhakikisha kila mshiriki wa mkutano huo wa siri anahusika kwa njia moja ama nyingine. Walihakikisha pia hakuna kifaa au chombo chochote cha kunasa sauti ama kusikiliza maongezi hayo ya siri.

Wajumbe wote wanne na bosi wao waliafikiana kuwa kila kitu kiko sawa na kila mmoja anakwenda kutekeleza walichoahoidiana.

"Nadhani wote tumeelewana sawa." Bosi waliuliza. Waliitikia kwa vichwa vyao.

"Sawa sasa nafunga mkutano. Tutakuwa tunawasiliana wakati kazi ikifanyika. Na mawasiliano yatakuwa ni ya mafumbo na si ya moja kwa moja. Abdallah tayari nimeshakufundisha lugha ya mafumbo tutakayotumia, sawa? Haya kwa kheri ya kuonana."

****************************************

Jina lake kamili ni Abesh Abdallah. Alizaliwa na wazazi mchanganyiko wa rangi, Mwarabu na Mluguru ya Matombo Morogoro.

Kwa sababu hakuwa mtoto halali wa ndoa wa baba yake Mwarabu, alilelewa na mama yake, tena ujombani.

Baba yake alikuwa na wake wawili wa ndoa ambao wote wa Waarabu wenzake, lakini alichepuka na mama wa Kiluguru na kumpata mtoto huyo Abesh.

Bahati nzuri ni kwamba, baba yake Abesh hakumkataa mtoto, ila hakutaka watu wajue, hasa Waarabu wenzake pamoja na wake zake, hivyo alimtunza kwa siri, alituma pesa ya matunzo na mambo mengine muhimu.

Alipofika kidato cha nne hakutaka tena kuendelea na masomo au kwenda chuo chochote kile, badala yake alitaka kufanya biashara.

Kwa sababu baba yake alikuwa mfanyabiashara mkubwa, alimpa basi moja kubwa la abiria, na lori moja ikiwa kama ni mtaji wake wa kuendesha maisha kwa sababu hatambuliwi kwenye familia yake.

Na kweli, miezi sita baadaye Mwarabu alifariki na mtoto wake wa nje, Abesh alianza maisha ya kuendesha biashara yake binafsi ambayo aliimudu vema.

Miaka mitatu baadaye alikuwa tayari ana mabasi saba ya abiria, malori matano, pamoja na biashara zingine kama maduka ya vipuri, pamoja na kuwa na mashamba makubwa ya kilimo cha biashara.

Akageuka kuwa tajiri mkubwa, akawa maarufu mjini Morogoro na kuwa na majina mengi ya utani ambayo yanafananishwa na watu wenye pesa nyingi ulimwenguni.

Maisha yake akayahamishia Dar es Salaam, maeneo ya Mbweni jijini Dar es Salaam. Upande wa pili wa maisha yake, alikutana na msichana mmoja mrembo matata, Grace.

Abesh alichanganyikiwa na msichana huyo. Lengo alitaka kumuoa awe mkewe. Hata hivyo imani zao zilikuwa tofauti. Lakini kwa sababu walipendana muafaka ukawa ni kuoana bomani kwa ndoa ya kiserikali.

Katika hali isiyo ya kawaida, mwaka mmoja baadaye Grace alikatisha mawasiliano na mpenzi wake Abesh.

Baada ya kumtafuta na kukusanya taarifa huku na huko, akagundua kuwa mpenzi wake amepata mpenzi mwingine ambaye pia ni tajiri kama yeye aitwaye Patiyo.

Abesh anamfahamu Patiyo kuwa ni tajiri mwenzake na mara kwa mara huwa wanakutana, kutaniana na kubadilishana mawazo kwenye vikao vyao, pamoja na mikutano ya wafanyabishara na serikali.

Hakutegemea kama jamaa huyo anaweza kumchukua mpenzi wake, ambaye wameahidiana mambo mengi na wametoka mbali.

Kibaya zaidi akasikia kuwa wiki ijayo mpenzi wake Grace anafunga ndoa na Patiyo na sherehe kubwa itafanyika kwanza kwenye jumba lake la kifahari maeneo ya Kibada, Kigamboni jijini Dar es Salaam, na baadaye kwenye hoteli moja ya kifahari katikati ya jiji la Dar es Salaam majira ya usiku.

Hiyo ni baada ya ndoa kufungwa kwenye kanisa la Mtakatifu Joseph katikati ya jiji la Dar es Salaam.

Hakuwa tayari kuona jambo hilo linafanyika mbele ya macho yake. Linafanyika kwa mtu ambaye ana kila kitu.

Ana pesa, ana ushawishi na kila aina ya zana inayoweza kusababisha anawazuia Grace na Patiyo kuwa mke na mume.

Ndipo alipobuni mpango kamambe wa kuwaangamiza mbele ya macho yake watoweke duniani ili abaki na amani moyoni. Kwa kutumia pesa zake na ushawishi aliweza kuwapata vijana wanne wanaoweza kufanya vitu tofauti, lakini lengo likiwa ni moja tu, Grace na Patiyo watoweke duniani kwa sababu hawana adabu.

Hawawezi kumdhalilisha, kumfedhehesha na kumtia aibu mtu kama yeye ambaye ametunikiwa utajiri, umaarufu na vitu vingine vinavyofanana na hivyo.

Abesh, ndiyo aliyekuwa akiongea na vijana hao ambao tayari wameshapewa maagizo ya nini wanachotakiwa kwenda kufanya.

Watu hao ameletewa na watu wake wa karibu na anaowaamini na kuambiwa kuwa hao ni vijana wenye uwezo wa hali ya juu wa kazi hizo.

Na hata alipozungumza nao na kupanga mikakati, ilionyesha kuwa ni kweli wameiva. Sasa kilichobaki ni kitu kimoja tu kuwamaliza Grace na Patiyo.

**Itaendelea Jumamosi**

# **MATANGAZO** MCHANGANYIKO



***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


## KUPOTEA KWA CHETI



**DICKSON DAGBERT NCHUMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha Chuo chenye namba **NS/675/0058/2015** kilichotolewa na CHUO CHA LITA MABUKI mwaka 2019.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MWA/NY/RB/153515/2020.**

115650102

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAHABU DANIEL JENGELA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0741-0117 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ITENDE SEKONDARI** mwaka 2009.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Control No: 9910811797277.**

115650402

## KUPOTE KWA KADI YA BAJAJ

BARAKA POLO MWANDEBWE anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj yenye namba za usajili MC 221 BFT aina ya TVS KING rangi ya kijani. Chassis namba MD6M14PK9G4A35762.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi MBE/MBE/RB/184181/2020.

115650702

## TANGAZO LA OMBI LA URAIA



**Bw IKRAM ULLAH, S.L.P 483 TANGA**

Tangazo limetolewa kwamba, mtu ambaye picha yake imetolewa hapo juu anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa mambo ya Ndani ya Nchi. Mtajwa kwa sasa ni raia wa **PAKISTANI** na anatokea nchi ya **PAKISTANI** pia anajishughulisha **AMEAJIRIWA KATIKA KAMPUNI**

Mtajwa amekuwepo hapa nchini tangia 2009 pamoja na kuishi **TANZANIA** Pia amewahi kuishi **PAKISTANI** kwamba mtu yeyote mwenye taarifa au sababu kwanini mwombaji asipewe uraia apeleke sababu hizo kwa maandishi yaliyosainiwa kwa kamisha Jenerali wa Uhamiaji, S.L.P 512 Dar es Salaam.

**Kumb. DN TA/TP/4318**
**kny. KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI**

156506

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:144..2019.**
**Mdai: EDSON NYANGWI ALBERT**
**DHIDI YA**

**Mdaiwa: SHUKURU RASHIDI**
**Kwa: SHUKURU RASHIDI**
**Ombi la Mdai: EDSON NYANGWI ALBERT**
**Madai ya: PESA SHILINGI 360,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 02 mwezi 03 mwaka 2020 saa 08:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 10 mwezi 02 mwaka 2020.

115650202

## HATI YA KIAPO

BIBIANA FRANCIS anatangaza kupotelewa kwa barua ya toleo (Letter of offer) ya kiwanja namba 726/1 Kitalu Q Mabawa ndani ya Jiji la Tanga na kwamba ni mmiliki halali wa kiwanja hicho baada ya kukabidhiwa na Amina Rashid mwaka 1996. Taarifa ya upotevu wa barua hiyo ya toleo umeripotiwa katika kituo cha polisi Chumbageni na kupewa RB No. TAN/TAN/RB/181417/2020.

Imeapwa na kuthibitishwa hapa Tanga na BIBIANA FRANCIS

Leo tarehe 26 mwezi 02, 2020.
Mbele yangu;

115651002


***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi Kwa***

***Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# CONTE: INTER ILISTAHILI USHINDI

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte aliisifia Inter Milan kwa kiwango walichokionyesha kwenye mchezo wa pili wa ushindi wa Ligi ya Europa dhidi ya Ludogorets kwenye hatua ya 32, wakicheza huku milango ikiwa imefungwa na kusema walistahili.

Mabao kutoka kwa Cristiano Biraghi na Romelu Lukaku yaliiwezesha Inter kupata ushindi wa magoli 2-1 kwenye Uwanja wa San Siro baada ya Cauly kuifungia la ufunguzi Ludogorets, ambao walifungwa 2-0 katika mchezo wa kwanza.

Hofu ya ugonjwa wa corona imetokea nchini Italia na mashabiki hawakuruhusiwa kuingia uwanjani na Conte amebainisha kwamba aliridhishwa na kiwango cha wachezaji wake.

"Nimecheza milango ikiwa imefungwa, lakini timu ilionyesha kiwango kizuri," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Hali ya hewa ilikuwa nzuri na mwanzo mambo yalionekana kuwa magumu, lakini hatimaye mambo yalikwenda sawa.

"Naweza kusema wachezaji walionekana kuwa kwenye ari nzuri na kwa uhakika walicheza kwa kiwango kizuri na tulistahili ushindi."

# Lampard kuwatema nyota Chelsea

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard anajianda kuwatema wachezaji nane kwenye kikosi chake wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, kipa Kepa Arrizabalaga ameshindwa kuonyesha ubora wake msimu huu na kupoteza nafasi kwa kipa Willy Caballero, ni miongoni mwa wachezaji wanaotajwa watatimuliwa na Lampard.

Viungo Ross Barkley na Jorginho pia wanaweza kuachwa pamoja na beki wa kushoto Marcos Alonso na Emerson, wakati Kurt Zouma, Willian na Pedro watakuwa wakiangaliwa mwenendo wao kuanzia sasa hadi mwisho wa msimu.

Hiyo imekuja baada ya kikosi cha Lampard kupokea kipigo cha mabao 3-0 katika Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora nyumbani na Bayern Munich, huku pia ikiwa nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu England.

Kipigo hicho kikubwa kwa Lampard kimeonyesha jinsi kikosi chake kinavyoitaji mabadiliko kabla ya kuanza kufikiria ubingwa.

Lampard tayari ameshatumia pauni milioni 37 kumsajili winga Hakim Ziech kutoka Ajax, ambaye atajiunga na klabu hiyo mwisho wa msimu.

Inaonekana bado anataka kusajili wengine wanne wakiwamo beki wa kushoto Ben Chilwell kutoka Leicester na kipa wa Atletico Madrid, Jan Oblak.





# Salah atabiriwa kuondoka Liver

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa zamani wa Manchester United, Gary Neville, amesema haamini kabisa kama Mohamed Salah atadumu pale Liverpool.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri amekuwa mchezaji muhimu wa Liverpool tangu alipojiunga na timu hiyo akitokea AS Roma misimu mitatu iliyopita.

Aliisaidia timu hiyo kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na msimu huu ameiweka kwenye nafasi nzuri ya kunyakua ubingwa wa Ligi Kuu England.

Lakini, Neville, aliyewahi pia kuwa kocha wa Valencia alisema anamwona Salah akienda kujiunga na ama Real Madrid au Barcelona ndani ya miaka michache ijayo.

"Sio kitu rahisi kumbadili mchezaji wa aina kama yake," alisema Neville.

"Nilisema miezi 18 iliyopita, nadhani Mo Salah ataondoka Liverpool.

"Nadhani ni jambo jepesi tu kuliona hilo kutokana na mashabiki wa Liverpool kushindwa kumpa Salah mapenzi anayostahili. Kuna ile hali naiona kabisa kwamba anataka kwenda kucheza Real Madrid, kwenda Barcelona, kwa uhamisho mkubwa.

"Hilo huwezi kumlaumu Mo Salah. Nilicheza na David Beckham, nilicheza na Ruud van Nistelrooy, nilicheza na Cristiano Ronaldo - wote hao walitaka kushinda Ballon d'Or, hivyo walitaka kwenda Real Madrid, walitaka kwenda kuonekana wakiwa na klabu hiyo.

"Ni hivyo. Tuseme ukweli tu, Real Madrid na Barcelona zimekuwa zikiwavutia wachezaji wengi wanapokuwa kwenye viwango bora."

HABARI MICHEZO

# Solskjaer asifia molari ya United

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anaamini wachezaji wake wameonyesha ishara ya kuimarika zaidi baada ya kuibuka na ushindi wa kuvutia kwenye Ligi ya Europa dhidi ya Club Brugge.

Mashetani wekundu hao walifuzu hatua ya 16 bora baada ya kuibuka na ushindi wa 5-0 dhidi ya Brugge iliyomaliza na wachezaji 10 pale kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Mabao mawili kutoka kwa Fred na mengine kutoka kwa Bruno Fernandes, Odion Ighalo na Scott McTominay yaliing'arisha United, ingawa Brugge walicheza kwa muda mwingi wakiwa na wachezaji 10 uwanjani baada ya Simon Deli kutolewa kwa kadi nyekundu.

Na Solskjaer alionyesha kufurahishwa na kiwango hicho cha United kuelekea kwenye mchezo wa jana Ijumaa na kuwango bora.

"Nafikiri sasa wachezaji wangu wameimarika zaidi," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Scott McTominay amerudi na nafikiri ameimarika. Fred, nilikuwa sina uhakika kama angekuwa poa kwa ajili ya mchezo ujao!"





# ARTETA AIKATIA TAMAA ARSENAL

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amekubali "itakuwa ngumu" kwa Arsenal kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya kupitia Ligi Kuu England baada ya kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Europa.

Pierre-Emerick Aubameyang alikosa bao sekunde za mwisho za mchezo huo na kuifanya Arsenal kutolewa na Olympiacos, ambao walinufaika na bao la ugenini baada ya sare ya 2-2, juzi Alhamisi.

Arsenal katika mchezo wa kwanza wa hatua hiyo ya 32 iliibuka na ushindi wa 1-0, lakini walilazimika kuingia kwenye muda wa ziada baada ya Pape Abou Cisse kuifungia Olympiacos kwenye mchezo huo uliopigwa uwanja wa Emirates.

Aubameyang alionekana kama angeweza kuipa matokeo Arsenal, lakini Youssef El-Arabi aliwanyamazisha na kuwatupa nje washikabunduki hao.

Kushinda taji la Ligi ya Europa kunaipa nafasi Arsenal ya kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao, lakini sasa wakabiliwa na mtihani mkubwa wa kumaliza kwenye nne bora katika Ligi Kuu England.

"Ni vigumu mno kumaliza kwenye nne bora kwa sababu ya msimamo wa Ligi unavyoonekana kwa sasa," amesema Arteta, ambaye alirithi mikoba ya kuinoa Arsenal kutoka kwa Unai Emery Desemba mwaka jana.

"Kitu cha muhimu kwa sasa ni kuhakikisha tunakuwa na matokeo mazuri katika kila mchezo wa Ligi Kuu. Kwanza tunatakiwa kukubaliana na kile kilichotokea na kuangalia mbele."

# *Rodgers ana matumaini Maddison kubaki Leicester City*

**LONDON,** England

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, ana matumaini James Maddison atasaini mkataba mpya licha ya kuhusishwa na mpango wa kutakiwa Manchester United.

Majaliwa ya Maddison yamezidi kutawala vyombo vya habari, huku nyota huyo wa Leicester akiripotiwa kutakiwa na miamba wa Ligi Kuu England, United.

United wamepanga kujaribu kutuma ofa yao kwa Maddison ili atue Old Trafford mwishoni mwa msimu huu, hata hivyo, Rodgers ana matumaini kiungo huyo wa England atasaini mkataba mpya wa kuendelea kukaa pale kwenye dimba la King Power.

"Mazungumzo yanaendelea na klabu na wawakilishi wa mchezaji," alisema Rodgers kuelekea kwenye mchezo wa jana Ijumaa dhidi ya Norwich City.

"Najua kijana ana furaha, anataka kuwa hapa na kuiona klabu ambayo amekua nayo na kuimarika nao. Natumaini itakuwa sawa."

Maddison amefunga mabao tisa katika mashindano yote kwa Leicester msimu huu, sita kati ya hayo yakiwa kwenye Ligi Kuu na ametoa 'asisti' tatu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 amejiimarisha yeye mwenyewe kuwa mmoja wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu tangu alipojiunga akitokea Norwich Juni 2018.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CITY YAJIPANGA KUMSAJILI HOLGATE

Ni katika mkakati wa Kocha Guardiola kuimarisha safu yake ya ulinzi kuelekea msimu ujao...

**MANCHESTER,** England

KATIKA kuhakikisha safu yake ya ulinzi inaimarika kuelekea msimu ujao, Manchester City inajiandaa kuwania saini ya beki wa kati wa Everton, Mason Holgate katika kipindi cha majira ya joto.

**Kikosi cha Pep Guardiola kimekuwa na wakati mgumu katika safu yake ya ulinzi msimu huu kutokana na beki wake tegemeo, Aymeric Laporte, kutumia muda mwingine nje ya uwanja akiiguza majeruhi.**

Holgate, ambaye ni beki na anaweza kucheza nafasi ya kiungo mkabaji, ni mchezaji muhimu anayeweza kuziba pengo la Manchester City na inaelezwa thamani yake inakaribia pauni milioni 30, limeandika gazeti la The Mirror.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23 amekuwa katika kikosi cha kwanza cha Blues tangu kuwasili kwa Carlo Ancelotti klabuni hapo na baada ya hapo amekuwa akishirikiana vema na Yerry Mina na Michael Keane. Pia amekuwa na mchango mzuri katika mechi zote alizocheza hata alipopangwa katika nafasi ya kiungo mkabaji.

Holgate alirejea Everton katika majira ya joto baada ya kucheza kwa mkopo katika mzunguko wa pili wa msimu uliopita katika klabu ya West Brom inayoshiriki Ligi ya Championship.

Mkataba wake na klabu hiyo unatarajiwa kumalizika mwaka 2022 na tayari alishaanza mazungumzo ya kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia timu hiyo.

Lakini City imeshamwona mchezaji huyo anaweza kukisaidia kikosi chake baada ya kipaumbele cha Guardiola msimu ujao ni kusajili mabeki.

Kuumia kwa Laporte, kulimlazimu kocha huyo kumtumia Fernandinho katika nafasi ya beki wa kati sambamba na Nicolas Otamendi ili kuchukua nafasi ya Laporte.

Hata hivyo, Mfaransa huyo alirejea katika kikosi hicho lakini alitolewa nje wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Real Madrid kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya uliochezwa Jumatano iliyopita.

Beki John Stones ambaye amekosa namba katika kikosi cha timu hiyo, hakuwa kwenye idadi ya wachezaji 18 licha ya kuwa fiti na kupelekea sintofahamu kuhusu hatima yake ndani ya klabu hiyo inayotumia Uwanja wa Etihad.

Gazeti la The Mirror liliandika na kupendekeza kuwa City inaweza kumtumia Stones, ambaye aliondoka Everton mwaka 2016, kurejea katika klabu hiyo kama sehemu ya mchakato wa usajili wa Holgate.

Everton ilimsajili Holgate kutoka Barnsley kwa dau la pauni milioni 2 mwaka 2015 na amekuwa akiichezea England katika timu za U-20 na U-21.

## ZISIKUPITE

### ARRIZABALAGA KUTUA CHELSEA

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, anajiandaa kusajili wachezaji wapya nane akiwamo golikipa wa Timu ya Taifa ya Hispania, Kepa Arrizabalaga (25), kiungo wa Italia, Jorginho (28) na kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Ross Barkley ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Sun)***

### UNITED ILIMKOSA DAVIES

MANCHESTER United ilishindwa kunasa saini ya beki wa kushoto wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Canada, Alphonso Davies (19), kwa dau la pauni milioni 2 mwaka 2017. ***(Times, subscription required)***

### ARSENAL, NEWCASTLE VITANI

ARSENAL, Newcastle na Southampton zinawania saini ya kiungo wa kati wa Hoffenheim na Timu ya Taifa ya Austria, Florian Grillitsch, ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Sport Bild, via Chronicle)***

### RUIZ ANUKIA MADRID

REAL Madrid inajiandaa kutoa dau la pauni milioni 58.8 ili kunasa saini ya kiungo wa Napoli na Timu ya Taifa ya Hispania, Fabian Ruiz (23). ***(Calciomercato - in Italian)***

### KANE KURUDI MAPEMA

STRAIKA wa Tottenham na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane (26), anaamini atarejea uwanjani Aprili baada ya majeraha yake kuendelea vema na hivyo kuanza kucheza mapema tofauti na ilivyotarajiwa. ***(Sun)***

### STURRIDGE ALIITOSA VILLA

STRAIKA wa zamani wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Daniel Sturridge (30), alikacha ofa ya kujiunga na Aston Villa katika dirisha la usajili la Januari kwa sababu alitaka kuisaidia klabu yake ya Trabzonspor kukata tiketi ya kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Fanatik, via Sport Witness)***

### FURRY KUWAFUNDA UNITED

BONDIA wa ngumi za kulipwa, Tyson Fury, amealikwa na Manchester United ili kuwaelezea wachezaji wa timu hiyo safari yake kuanzia maisha yake ya chini hadi alivyofanikiwa kutwaa mkanda wa dunia unaotambulika na WBC dhidi ya Deontay Wilder. ***(Metro)***

### KARIUS AIANGUKIA LIVERPOOL

GOLIKIPA Loris Karius (26), amesema anataka kuona Liverpool inamwacha aondoke kama mchezaji huru na baadaye atabadilisha uhamisho huo wa mkopo kwenye klabu ya Besiktas ya Uturuki na kusaini mkataba wa kudumu. ***(Fotospor, via Turkish Football)***

### EVERTON ILIIBANIA SPURS

MABOSI wa Everton walikataa kupokea ofa kutoka Tottenham iliyokuwa inahitaji kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya England, Michael Keane (27), mwishoni mwa mwaka jana. ***(Football Insider)***

### GOMES AITEGA UNITED

MANCHESTER United bado ina matumaini ya kuona kiungo wa Timu ya Taifa ya vijana ya England (U-20), Angel Gomes, atabakia Old Trafford licha ya mkataba wake wa sasa kumalizika ifikapo Juni mwaka huu. ***(Manchester Evening News)***

## Manara awaita Simba Arumeru

**Na Saada Akida**

HUKU timu yao ikiendelea kuongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara anatarajiwa kufungua tawi jipya la klabu hiyo katika Wilaya ya Arumeru jijini Arusha, hapo kesho.

Akizungumza na gazeti hili jana, Manara, alisema maandalizi ya uzinduzi wa tawi hilo yamekamilika na wanawaomba mashabiki wa Simba walioko Arusha kujitokeza ili wapate kadi za mashabiki.

Manara alisema kuwa mchakato wa kufungua tawi hilo ni mwendelezo wa kuboresha daftari la wanawachama wa Simba na limekuwa likiendelea katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

"Jumapili hii baada ya kumalizika kwa Kilimanjaro Marathon, mchana nitakuwa Wilaya ya Arumeru nikiwa mgeni mwalikwa wa kufungua tawi la Simba wilayani hapo, watu wa Arusha na Kilimanjaro hususani WanaSimba mliopo Arumeru tukutane kuijenga klabu yetu," alisema Manara.

Manara na Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki wa Simba, Hashim Mbaga, wanaendelea na mchakato huko katika mikoa mbalimbali katika siku za hivi karibuni.

## KMC kuboresha benchi la ufundi

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa KMC FC umesema utaendelea kuboresha benchi lake la ufundi ili kuhakikisha kikosi chao kinapata matokeo mazuri kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazoendelea hapa nchini.

Mrundi Haruna Hererimana ndiye kocha mkuu wa timu hiyo ambayo ina pointi 21, iko katika nafasi ya 19 kwenye msimamo wa ligi hiyo huku Singida United yenye pointi 12 ikiburuza mkia.

Mwenyekiti wa Bodi ya timu hiyo, Benjamini Sitta, aliliambia gazeti hili uamuzi wa kuondoa na kuajiri watendaji katika benchi la ufundi unalenga kusaka matokeo mazuri na hawatasita kubadilisha makocha mpaka pale watakaporidhika na matokeo.

Hata hivyo Sitta alisema anaridhishwa na kasi mpya inayoonekana katika kikosi chao na anaamini ndani ya muda mfupi, matunda wanayoyatafuta wataanza kuyaona.

"Timu ikipata mwendo mzuri wa kushinda, itapata kasi ya kushinda, tumeanza kuwapa mawaidha ili kuwaboresha, katika hilo, tunaendelea kumtoa huyu, kumleta mwingine, ili kuona mambo yanaenda sawa, lakini kocha pia tumemwekea malengo," alisema Sitta.

KMC leo itaikaribisha JKT Tanzania wakati Machi 7, mwaka huu itawaalika Mbao FC kutoka jijini Mwanza.

# SHIME AJIPANGA KUIVAA UGANDA KWA TAHADHARI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), Bakari Shime amesema mchezo dhidi ya Uganda utakuwa mgumu kutokana na wapinzani wao kutokubali kutolewa mara mbili na Tanzania katika mashindano mawili tofauti.

Tanzania inatarajia kuikaribisha Uganda katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia za U-17 huku ikiwa na kumbukumbu ya kuwatoa wapinzani hao katika michuano ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za baadaye mwaka huu za Kombe la Dunia kwa umri chini ya miaka 20 (U-20).

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Shime alisema mechi hiyo itakuwa ya upinzani mkubwa kutokana na timu hizo kukutana awali na wachezaji wake kufahamiana vema.

**Shime alisema anafahamu Uganda watakuja wakiwa na mipango ya kulipa kisasi na kikosi chake kimejipanga kushuka uwanjani kupambana ili kupata matokeo mazuri katika mchezo huo wa nyumbani.**

"Waganda ni wapinzani wetu, huu mchezo utakuwa na ushindani mkubwa, ukiangalia wachezaji saba wa U-17 wa Uganda wako kikosi cha kwanza timu ya U-20, halikadhali na kwetu tuna wachezaji sita wanacheza U-20, tumekutana katika mechi za hivi karibuni, tunajuana vema," alisema Shime.

Aliongeza kikosi chake kiko tayari kukabiliana na wapinzani wao na wamejiandaa kupeperusha vema bendera ya nchi kwenye ardhi ya nyumbani.

Naye nahodha wa timu hiyo, Irene Kisisa alisema kikosi chao hakina majeruhi na kila mchezaji yuko imara kuwasubiri Waganda katika mechi hiyo itakayochezwa kuanzia saa 9:00 mchana.

"Tumejiandaa vya kutosha, Jumapili tunaenda kupambana kwa kuzingatia maelekezo ya benchi la ufundi, tutahakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema Irene.

Tanzania ilifika hatua hiyo baada ya kuwatoa Burundi wakati Uganda yenyewe iliwaondoa Ethiopia.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17, wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi dhidi ya wenzao kutoka Uganda itakayochezwa kesho. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Simba Queens yaongoza ligi

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Simba Queens, inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania baada ya kupata ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Alliance Girls katika mchezo wa ligi hiyo uliochezwa kwenye Uwanja wa Mo Arena juzi jijini Dar es Salaam.

Ushindi huo umeifanya Simba Queens ifikishe pointi 26 na kukaa kileleni katika ligi hiyo ikifuatiwa na Alliance Girls yenye pointi 25 huku Ruvuma Queens wenye pointi 24 wakiwa kwenye nafasi ya tatu.

Mabao ya Simba Queens katika mechi hiyo yalifungwa na Mwanahamisi Omary ambaye alipachika mawili huku Opa Clement na Amina Hamza walifunga bao moja kila mmoja.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo, Yanga Princess ilipata ushindi wa mabao 8-1 dhidi ya Marsh Queens na kufikisha pointi 15 zilizowaweka katika nafasi ya tano katika msimamo huku mabingwa watetezi JKT Queens walioko nafasi ya nne wakiwasambaratisha Kigoma Sisterz mabao 8-0 na kufikisha pointi 22.

Ruvuma Queens iliwaadhibu Tanzanite SC magoli 4-0 huku Mlandizi Queens wakishinda mabao 2-1 dhidi ya TSC Queens ya jijini Mwanza na Baobab Queens iliyokuwa ugenini mkoani Iringa ilipata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya wenyeji Panama Girls.

Tanzanite SC na Panama Girls ambazo kila moja zina pointi tatu baada ya kushuka dimbani mara 10, ndio zinaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 12 na inayochezwa kwa mtindo wa nyumbani na ugenini, huku ikitarajiwa kuendelea tena Machi 4, mwaka huu.


# Michezo

Jumamosi Februari 29, 2020

Nipashe




Solskjaer asifia molari ya United UKURASA 29



Beki wa Arsenal, Hector Bellerin (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Olympiacos, Kostas Tsimikas katika mechi ya hatua ya 32 Bora ya Ligi ya Europa iliyochezwa kwenye Uwanja wa Emirates juzi usiku. Arsenal ilifungwa mabao 2-1 na kutolewa katika michuano hiyo kwa matokeo ya jumla ya magoli 2-2.
**PICHA: MTANDAO**

## Simba yatamba KMC hachomoki

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema atateremsha kikosi kamili kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC itakayochezwa kesho usiku kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Simba iliwaacha baadhi ya nyota wake wa kikosi cha kwanza katika mechi yake iliyopita ya Kombe la FA dhidi ya Stand United, ambayo ilichezwa Shinyanga na kupata ushindi wa penalti 3-2 baada ya sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90.

Sven alisema kwa sasa amekiandaa kikosi chake kupata ushindi katika mechi ya kesho na baada ya mchezo huo ndiyo watajipanga kufikiria timu nyingine.

"Tuna mechi tatu muhimu, kwanza ninaifikiria KMC, halafu Azam na baadaye Yanga, tutaangalia mechi moja baada ya nyingine, tunahitaji ushindi Jumapili, ushindi wa mechi hii utaendelea kutupeleka kwenye malengo," alisema Sven.

Aliongeza wanatarajia mchezo huo utakuwa na ushindani lakini wachezaji wake wanatakiwa kupambana kusaka matokeo mazuri.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema amewataka mashabiki wa timu hiyo kuhakikisha wanakuwa na kadi za mashabiki ili kuwa kwenye nafasi ya kutambulika uanachama.

Manara alisema kwa mfumo huo utawasaidia mashabiki na wanachama wa Simba kupata huduma katika maduka mbalimbali hapa nchini na kueleza gharama halisi ya kadi hizo ni Sh. 24,000.

# Yanga, Alliance hapatoshi

## Mkwasa afunguka 'gari' lao limewaka, lakini watacheza kwa tahadhari ili kuhakikisha pointi tatu...

**Na Somoe Ng'itu**

HATUKUBAHATISHA! Hayo ni maneno ya Yanga kuelekea mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Alliance FC kutoka Mwanza inayotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**Yanga itashuka dimbani katika mechi hiyo ikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare nne mfululizo katika mechi za ligi huku Alliance ikiwa na kumbukumbu ya kumchapa Mwadui FC mabao 4-1.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Boniface Mkwasa, alisema timu yake iko tayari kwa mchezo huo unaotarajiwa kuwa na ushindani na wachezaji hawana hofu ya aina yoyote.

Mkwasa alisema wamejipanga kuendeleza kasi ya ushindi na wanaamini wakifanya vizuri katika mechi zao zinazofuata, wana nafasi ya kuutwaa ubingwa wa ligi ambao sasa unashikiliwa na watani zao Simba.

"Maandalizi yetu ni mazuri, timu haina hofu yoyote kuelekea mechi ya kesho (leo), kama baadhi ya mashabiki wenye lengo la kuwavuruga wachezaji wao kisaikolojia wanavyodai, na kuelekea pia katika mchezo wa dhidi ya Simba tutakaocheza Machi 8, mwaka huu," alisema Mkwasa.

Kocha huyo alisema wanaifahamu Alliance FC na kuitambua ni moja ya timu zinazoundwa na wachezaji wenye vipaji na wanaocheza kwa kasi, hivyo wamejipanga kukabiliana na changamoto hiyo.

Aliongeza ushindi walioupata katika mechi dhidi ya Gwambina FC katika mashindano ya Kombe la FA, imewaongezea morali wachezaji wake na kila mmoja amejiandaa kuisaidia timu kuondoka na pointi tatu.

"Tutaingia uwanjani kwa tahadhari kubwa, tunaiheshimu Allinace na kamwe hatuwezi kuibeza, mechi zote ni ngumu na hii inatokana na namna timu zilivyojipanga kwa kuhofia kushuka daraja," Mkwasa alisema.

Alieleza anafahamu mashabiki wa Yanga wanahitaji kuona timu yao inapata ushindi na kuona burudani ambayo itawarejesha kwenye mbio za kuwania ubingwa baada ya kukata tamaa iliyotokana na matokeo ya sare nne walizopata katika mechi zilizopita.

Nahodha wa Yanga, Juma Abdul, aliliambia gazeti hili wachezaji wote wako tayari na kamili kupambana na hatimaye kupata pointi tatu.

"Hakuna mechi nyepesi, lakini tumeshaona upungufu wetu, tutataka kumaliza unyonge, tumejipanga kurejesha heshima, tunaamini tutafanikiwa kupata tunachokitafuta," alisema beki huyo.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Mwadui FC dhidi ya Coastal Union, Kagera Sugar vs Tanzania Prisons, Ruvu Shooting vs Mbao FC, Lipuli vs Namungo, Biashara United vs Mbeya City, Mtibwa Sugar vs Ndanda na JKT Tanzania wataialika Azam FC.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >